epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

Jumatatu Oktoba 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581827

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**EDERSON ACHAMBUA NGUVU YA GUARDIOLA**

UKURASA WA 3

**ACT** yataja dosari tano uandikishaji Uchaguzi S/Mitaa

UKURASA WA 4

**Mfugaji** auawa kwa kupigwa risasi na polisi



UKURASA WA 5

**Wananchi** wagawana mali za mtuhumiwa mauaji ya mtoto, nguo hadi matofali ya jengo

# Malecela: Sitosahau Nyerere aliponituma kumwona Idi Amin

• **Aliona** maisha rehani, Amin alimzungusha mitaani Kampala wakiwa wawili katika gari, akafanikiwa kutorosha wanafunzi wa kitanzania... *Endelea ukurasa 9*



John Malecela

Idi Amin

UKURASA WA 15

**NEMC YAONYA KUFUNIKA CHAKULA KWA KUTUMIA MIFUKO YA PLASTIKI**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa onyo kwa mama ntilie...

UKURASA WA 15

**WASIOJULIKANA WABOMOA MADARASA YA SHULE MPYA**

TAHARUKI imetanda miongoni mwa wakazi wa kata ya Tembela, jijini Mbeya, baada ya watu wasioju-

## Warioba: Nyerere alilenga matatu; simulizi alipokutana na mwalimu wake

UKURASA 10 & 16



## Rais Samia aahidi kununua vifaa vya kisasa utafiti madini

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAANIKA SIRI INAPOIZIDI SIMBA** UK.24

**KATUNI** UK.6

# ACT yataja dosari tano uandikishaji wa S/Mitaa

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kimebaini dosari tano katika mchakato wa uandikishaji wapigakura kwenye Daftari la Wakazi, kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika mwezi ujao.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu alitaja dosari hizo jana wakati anazungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Alitaja upungufu huo tangu kuanza uandikishaji Oktoba 11 ni pamoja na TAMISEMI kutofanya uhamasishaji wa kutosha, ili kuongeza hamasa ya wananchi kujiandikisha.

“Licha ya kutengewa bajeti ya Sh. bilioni 17.79 kwa ajili ya kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, TAMISEMI haijafanya jitihada zozote za maana kuhamasisha wananchi,” alisema Ado.

Ado alitaja dosari ya pili ni baadhi ya wasimamizi wa vituo kukataa kutoa idadi ya wananchi waliojiandikisha katika siku husika kwa mawakala hasa namba na jina la mwisho kuandikishwa pindi mchakato unapoahirishwa jioni, ili siku inayofuata kujiridhisha kuwa hakuna majina yaliyoongezwa kinyemela.

Alisema jambo la tatu ni madai ya kuandikishwa watoto na watu wasio na sifa za kuandikishwa, akisisitiza kuwa chama chao kimepokea taarifa za watoto, hasa wanafunzi wasiotimiza umri wa kupigakura, wanakusanywa kwenda kuandikishwa vituoni.

Alidai ukiukwaji huo wa taratibu za uchaguzi umefanyika Halmashauri ya Ubungo (mtaa wa Luguruni, kata ya Kwembe).

Jambo la nne, Ado alisema ni TAMISEMI kutoshusha maelekezo ya kuruhusu mawakala kuendelea kupokewa vituoni siku yoyote ya uandikishwaji, kwa kuwa uandikishwaji unaendelea.

Ado alitaja dosari ya tano ni kuwapo alichokiita “vituo bandia vya uandikishaji wapigakura”, licha ya mwongozo wa uandikishaji kuweka bayana kuwa, kwa mamlaka za vijijini, uandikishaji utafanyika kwenye vitongoji. Alidai baadhi ya wasimamizi wa vituo wameanzisha vituo zaidi bila kuwashirikisha wadau.

“Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Kilwa, ameongeza vituo vitatu vya Nyuni, kata ya Songosongo, Bwidi na Mbunju katika kata ya Miguruwe.

“Kituo cha Nyuni kipo katika kisiwa kidogo cha wavuvi kisicho na makazi ya kudumu. Licha ya wadau kupinga na msimamizi wa uchaguzi kuahidi kusimamisha uandikishaji kwenye maeneo hayo, uandikishaji unaendelea,” alidai.

Ado alisema ACT inatoa wito kwa TAMISEMI kuongeza kasi ya uhamasishaji wananchi kujiandikisha, hasa kwa kutumia njia zinazowafikia wananchi wengi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI
OSHA

KUMBUKUMBU YA MIAKA 25 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA

HAYATI, MWALIMU
J.K.NYERERE



Bodi ya Ushauri (MAB), Menejimenti na Watumishi wote wa **Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),** tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kuadhimisha kumbukumbu ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwl. Julius K.Nyerere. Tutamkumbuka na kumuenzi daima kwa uongozi wake dhabiti ulioleta umoja, mshikamano, uzalendo na Amani miongoni mwa watanzania wote.

***OSHA tutaendeleza yale aliyoayaanzisha na kuyasimamia kwa kufanya kazi kwa bidii huku tukiwaongoza watanzania kuzingatia Usalama na Afya katika shughuli zao za kila siku.***

P.O. BOX 519, Dar es salaam, Tanzania.
TEL: +255-22-2760548, FAX: (0)22 2760552;
E-mail:info @ osha.go.tz, WEBSITE:www.osha.go.tz

TOLL FREE: 0800110091 / 0800110092 | @ tanzania Osha | Occupational safety and health Authority-OSHA
osha_tanzania_official | 0735 - 757 675 | YouTube OSHATV Online


# Rais Samia aahidi kununua vifaa vya kisasa utafiti madini

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema ni asilimia 16 tu ya madini yote yanayopatikana nchini na kuuzwa ambayo yamefanyiwa utafiti.

Kutokana na hali hiyo, amesema serikali imejipanga kuwekeza katika ununuzi wa vifaa, zikiwamo helkopta, vitakavyosaidia kufanya utafiti nchi nzima kutambua maeneo yenye madini na kiwango chake.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana, mkoani Geita wakati akifunga maonesho ya saba ya teknolojia ya madini na kueleza kuwa baada ya uwekezaji huo, serikali itakuwa na uwezo wa kwenda nje na kuvutia uwekezaji katika sekta hiyo.

“Hapo tutakuwa na uhakika wa kiasi gani cha madini kimo ndani ya nchi, hivyo tumeongeza fedha nyingi kwa ajili ya kufanya utafiti, ili tuwe na takwimu nzuri na za uhakika katika rasilimali yetu hii ya madini,” alisema.

Rais alisema uwekezaji huo wa serikali utaleta matokeo mazuri kama ilivyokusudiwa na kuwa tayari yameanza kuonekana katika mchango wa Pato la Taifa. Kwa mwaka 2023, mchango wake ulikuwa asilimia tisa kutoka asilimia 7.2 huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025.

Alisema sekta hiyo inaongoza kwa kuliingizia taifa fedha za kigeni na kuwa kwa mwaka 2023 iliingiza asilimia 56 ya fedha zote za kigeni, hivyo kuahidi kuwa serikali itaendelea kuipa kipaumbele kwa kuwainua wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa sambamba na kuwa karibu nao.

Alisema ongezeko hilo limetokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali, ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji pamoja na upatikanaji teknolojia ambako kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), serikali imefanya ununuzi wa mitambo mikubwa 15 ya uchorongaji miamba.



“Mitambo mitano imeshafika nchini na 10 ipo njiani inakuja, ili kuwarahisishia wachimbaji kufanya kazi kwa uhakika na kuwaepusha na hasara,” alisema.

Rais pia alisema mitambo hiyo itakapofika itatawanywa katika maeneo yote ya uchimbaji, akimwagiza waziri kutenga mitambo miwili mahususi kwa ajili ya wachimbaji vijana na mtambo mmoja kwa wachimbaji wanawake.

Pia alisema serikali imetenga Sh. bilioni 200 kama dhamana ya mikopo, ili kuwawezesha wanunuzi wa madini kukopa na kufanya kazi zao vizuri.

“Vivyo hivyo Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeweka Sh. trilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa dhahabu, hivyo yote hiyo ni mipango ya kuhakikisha tunakuza madini na kwa wakati huo tunabaki na akiba ya dhahabu kama dhamana ya utajiri wetu kwa siku zijazo,” alisema.

Rais alisema masoko ya madini yaliyosogezwa kila mkoa pamoja na vituo vya kununulia madini katika maeneo yanakochimbwa madini, sasa kukiwa na masoko 44 katika mikoa yote na vituo 103 vya kununulia madini, yamesaidia kuwapo mzunguko mzuri wa biashara.

“Kwa mwaka 2023/24, madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni mbili yaliuzwa kupitia masoko ya madini na kuwezesha serikali kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 180 kutokana na masoko hayo mbali na mapato mengine yanayokusanywa na wizara,” alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema serikali imefuta leseni zaidi ya 2,000 zilizokuwa zimehodhiwa kwa muda mrefu, wakiwamo wawekezaji wazawa waliokuwa waliohodhi leseni zenye ukubwa ya ekari zaidi milioni 13, ambazo watagawiwa wachimbaji wadogo kwa kuweka kipaumbele kwa vijana na wanawake.

Mavunde alisema Wizara ya Madini ina mpango wa MBT unaolenga kuwafikia vijana na wanawake.

“Sh. bilioni 231 zimetengwa na kuelekezwa kwenye Taasisi ya Utafiti wa Madini (GST) na kwamba maabara kubwa mbili; moja itajengwa Dodoma na maabara za kanda; moja itajengwa Mkoa wa Geita kwa ajili kuwasaidia wachimbaji kupima sampuli,” alisema Mavunde.

Rais wa Shirikisho la vya Vyama vya Wachimbaji wa Madini Tanzania, John Bina, alimwomba Rais Samia kuweka msamaha wa kodi, kwa vifaa vya uchimbaji madini ya dhahabu vinavyonunuliwa na wachimbaji wadogo, ili kuwawezesha kuchimba madini kisasa.

Alisema kupitia kikao chao kilichofanyika Dodoma hivi karibuni, walikubaliana wachimbaji wadogo wa madini na wafanyabiashara kuizuia BoT asilimia 20 ya madini ya dhahabu, hivyo kutaka benki hiyo iwe imara kuviwezesha viwanda vya kusafisha madini vipate mtaji, ili zifanye kazi kwa uhakika.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, alisema maonesho hayo yanakuwa kila mwaka na kwamba mwaka jana, walikuwa na washiriki 350 kutoka ndani na nje na kwa mwaka huu washiriki wameongezeka na kufikia 856.

“Sh. bilioni saba zimetengwa na serikali kupeleka umeme kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ambao wamezalisha zaidi ya kilo 16,262 zenye mauzo ya Sh. trilioni 2.2,” alisema Shigella.

***Imeandaliwa na Alphonce Kabilondo (GEITA), Neema Emmanuel na Vitus Audax (MWANZA).***

## HABARI KITAIFA

# Mbunge ataka muswada Sheria ya Ndoa upelekwe bungeni

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa Singida Mjini, Mussa Sima ameomba Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Wenye Mahitaji Maalum, kupeleka bungeni muswada wa kurekebisha Sheria ya Ndoa, ili kumlinda mtoto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni.

Sima ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani yaliyoandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na kushirikisha wasichana na wadau kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Sima alisema kuwa huu ndio wakati mahususi kwa wizara hizo za kisekta zinazohusika katika eneo hilo, kufanyia kazi sheria hiyo.

"Kazi kubwa ya wabunge ni kushauri serikali, nitoe wito sasa kwa mawaziri wa kisekta, huu ndio wakati wa kutuletea muswada, tuchakate, upelekwe bungeni na wabunge wapate nafasi ya kuchangia, kupata mawazo mbadala ili jambo hili litekelezeke.

"Sasa hivi kuna utata sana kuhusu umri sahihi wa mtoto wa kike kuolewa, tunaona mtandao wa elimu Tanzania na wadau wengine wameamua kwa dhati kuleta chachu ya mabadiliko ya kutaka mtoto wa kike atimize ndoto yake, wakihamasisha juu ya ulinzi wake dhidi ya ukatili na unyanyasaji," alisema.

Kuhusu baadhi ya wazazi kuwatumia watoto wao wa kike kama kitega uchumi, Sima aliwataka wabadili mitizamo yao na kuwawezesha watimize ndoto zao za kufika mbali kielimu.

Mratibu wa TEN/MET, Martha Makala, alisema wanaendelea kuelimisha jamii kuhakikisha watoto wanakwenda shuleni na kupata haki yao ya elimu.

"Wazazi, walezi na jamii pia tuhakikishe watoto wanapata chakula shuleni. Kama sisi tunavyokula majumbani, ndivyo hivyo tuwathamini watoto wetu, ili wasikae na njaa na itawashawishi wapende kubaki shuleni na wasiingie kwenye vishawishi vingine kwa sababu ya njaa," alisema Martha.

# Mfugaji apigwa risasi na polisi

**Na Said Hamdani,** LIWALE

MKAZI wa kijiji na kata ya Mirui, wilayani Liwale, mkoani Lindi, Herman Budam (17), amefariki dunia na mwingine Mbekwa Lala (20) kujeruhiwa kwa risasi na askari polisi, baada ya kutokea kinachodaiwa "vurugu za kutaka kuchukua mifugo yao iliyokamatwa na jeshi hilo".

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, mashuhuda wa tukio hilo, wazazi na ndugu, walisema tukio hilo lilitokea Oktoba 9 mwaka huu, saa 10:30 jioni.

Mashuhuda walijitambulisha kwa majina ya Rashid Muhutusa, Jeremia Muhatsu na Michael Jacobo, walidai kuwa siku hiyo, vijana hao wakiwa wanachunga mifugo ya baba yao Herman Muhenndi, askari polisi waliokuwa kwenye operesheni ya kuzuia na kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji walifika kijijini huko.

Walidai kwamba katika operesheni hiyo askari walikamata ng'ombe 800 waliokuwa katika maeneo yasiyo rasmi wakilishwa, hali iliyowakasirisha wafugaji hao, hivyo kukusanyika wakiwa na silaha za jadi na kukabiliana na askari hao.

"Hali hiyo ilizua vurugu kubwa kati ya wafugaji na askari waliokuwa kwenye operesheni na kusababisha kifo na majeruhi," walidai.

Walidai kwamba ndugu na jamaa wa kijana huyo wamegoma kuchukua mwili wa kijana huyo, kwa madai ya kutoridhishwa na kile walichokita "uonevu waliofanyiwa na askari polisi".

Herman Muhenndi, baba wa kijana aliyeuawa, akizungumza kwa niaba ya wafugaji wenzake, alidai wanalimiliki eneo hilo kihalali, baada ya kuuziwa na uongozi wa serikali ya kijiji husika.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Kanda ya Kusini, Daudi Kalele na ndugu wa marehemu walidai hawako tayari kuchukua mwili wa kijana wao hadi Mawaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Yusuf Masauni na wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega watakapofika kijijini huko kutaja waliowatuma askari hao.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Goodluck Mlinga, alipoulizwa kuhusu kuwapo zoezi hilo katika eneo lake la utawala, alithibitisha kulitambua na kueleza tayari wafugaji wametengewa ekari 100,000 huko Kimambi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za ufugaji.

Hata hivyo, Mlinga alisema kuwa licha ya kuwapa ekari 100,000 kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za mifugo, baadhi yao wamekuwa wanakaidi na kulisha mifugo katika mashamba na mazao ya wakulima, hivyo kusababisha vurugu zinazozalisha mauaji kwa wananchi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP John Imori, alithibitisha kuwapo tukio hilo, akidai askari walikuwa katika operesheni kuzuia na kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji, wakikamata ng'ombe 800 waliokutwa eneo lisiloruhusiwa kwa shughuli za ufugaji.

Kamanda huyo alisema katika vurugu hizo, mfugaji aliyemtaja kwa jina la Nekava Ghutam, mkazi wa kijiji cha Mirui, alijeruhiwa kwa risasi japo alifanikiwa kukimbia kutoka eneo la tukio.


**KASAROBA COMPANY LIMITED**

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA **LK MICROFINANCE** TUTAUZA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA, NYUMBA ILIYOWEKWA KAMA DHAMANA YA MKOPO AMBAPO MTEJA HUSIKA AMESHINDWA KULIPA MKOPO WAKE KWA MUJIBU WA MKATABA HUSIKA. HIVYO BASI IFAHAMIKE KUWA UTAKAPOPITA MUDA WA SIKU KUMI NA NNE (14) DHAMANA HUSIKA ITAUZWA KWA NJIA YA MNADA KWA SIKU HUSIKA ILIYOPANGWA, MNADA UTAFANYIKA SEHEMU NYUMBA HUSIKA ILIPO SIKU NA TAREHE KAMA ILIYOTAJWA KWENYE JEDWARI HAPO CHINI.

| NA | JINA LA MTEJA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | HATI YA DHAMANA | SIFA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | HADIA RASHID JUMA | NYUMBA IPO BOKO CHAMA | HATI YA MAUZIANO | NYUMBA NI KUBWA, NA YA KISASA | JUMANNE 29/10/2024 SAA 5 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA 75% NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14).
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA LA MNUNUZI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE.
3. KWA MAWASILIANO **MOB: 0718 643 008, 0767 005 035.**

**WOTE MNAKARIBISHWA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

**MIAKA 25 YA KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE**

MIAKA 25 1999 – 2024



*The Late Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Father of Nation*

Uongozi na wafanyakazi wa Chama cha Walimu Tanzania, wanaungana na Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania Wote kuadhimisha miaka 25 ya kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

CWT tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa weledi ili kuchangia katika maendeleo ya nchi.

*"Mshikamano daima ndio mkombozi wetu"*

**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**

**S.L.P 3077, DODOMA**

**Email: info@ttu.or.tz**

**Website: www.ttu.or.tz**

# Zahanati iliyotumia tochi ya mlinzi kutibu wagonjwa yapata umeme



Mwonekano wa ndani wa Zahanati ya Rwakaremera baada ya kupata nishati ya umeme. **PICHA: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia,** NGARA

SIKU sita baada ya kuripotiwa na gazeti hili Zahanati ya Rwakaremera kutokuwa na umeme, hatimaye serikali imepeleka huduma hiyo katika zahanati hiyo.

Septemba 5, mwaka huu, Nipashe iliripoti kuwa zahanati hiyo ya kijiji cha Rwakaremera, kata ya Kasulo, wilaya ya Ngara, mkoani Kagera haikuwa na umeme, hivyo nyakati za usiku watoa huduma wake kulazimika kuhudumia wagonjwa wakitumia tochi ya mlinzi wa zahanati.

Ni zahanati iliyoasisiwa na wakazi wa kijiji hicho waliochangishana Sh. 20,000 kwa kila kaya na kupata jumla ya Sh. milioni 30 na kuanza ujenzi wake mwaka 2021, kwa kujenga boma na baadaye serikali ikatoa Sh. milioni 50 za ukamilishaji wake na mwaka uliofuata ikaanza kutoa huduma.

Yusufu Katura, Diwani wa Kasulo anasema kuwa Septemba 11, mwaka huu, ikiwa ni siku sita baada ya Nipashe kuripoti kuhusu hali hiyo inayokinzana na miongozo ya kitaifa ikiwamo Sera ya Afya (2007), serikali ilipeleka huduma ya umeme katika zahanati hiyo.

Anasema upatikanaji nishati hiyo katika zahanati hiyo umesaidia kuondoa malalamiko ya wananchi ya kukosa huduma nyakati za usiku, wanapokuwa na wagonjwa wa dharura, wakiwamo wajawazito.

Diwani Katura anasema kuwa kila kikao cha Baraza la Madiwani, alikuwa anawasilisha hoja kuhusu suala la zahanati hiyo kutokuwa na umeme na kupewa ahadi zisizotekelezwa kwamba ingeunganishiwa huduma hiyo.

"Gazeti Nipashe lilipoandika kwamba zahanati yetu haina nishati ya umeme, suala hili lilifanyiwa kazi haraka na sasa hakuna tena malalamiko ya wananchi.

"Septemba 5, mwaka huu, Nipashe ilitoa taarifa juu ya namna wagonjwa wanavyopata adha kwa kuhudumiwa kwa kutumia tochi ya mlinzi wa zahanati. Siku iliyofuata (Septemba 6, 2024) mashimo ya nguzo yalianza kuchimbwa na kuwekwa nguzo na tarehe 11 Septemba umeme uliwaka kwa mara ya kwanza kituoni na huduma zinaendelea kutolewa," Diwani Katura anapongeza hatua zilizochukuliwa.

Anabainisha kuwa zahanati hiyo inahudumia vitongoji vya Kamula na Ngoma, kijijini Rwakaremera.

"Sasa huduma za afya zimeboreshwa na wagonjwa wanapata matibabu mchana na usiku. Changamoto iliyopo hivi sasa katika zahanati hiyo ni uhaba wa mabenchi.

"Tutakaa kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ili kuangalia namna ya kutatua changamoto ya uhaba wa mabenchi kwa ajili ya kukaa wagonjwa, kilio chao kikubwa kimeshatatuliwa," anasema.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Dk. John Samweli, anasema kupatikana nishati ya umeme kituoni, kumesaidia kuwaondolea adha ya kutumia tochi ya mlinzi na simu janja zao nyakati za usiku, akiitaja ilikuwa kero kuu kwa wananchi, hasa wajawazito na watoto waliohitaji huduma za dharura kituoni usiku.

"Umeme kwa mara ya kwanza umewaka kwenye zahanati hiyo Septemba 11, mwaka huu na wananchi walikuwa wakishuhudia na walifurahi sana, walisikika wasema 'hatutahudumiwa kwa tochi ya mlinzi tena'. Sisi wenyewe umeme umeturahisishia utoaji huduma," anasema.

Dk. Samweli anafafanua kuwa hivi sasa zahanati hiyo ina watoa huduma wanne ambao ni mtaalamu wa maabara, muuguzi, ofisa afya msaidizi na Mganga Mfawidhi.

"Hatutaki tena kusikia wananchi waliojitoa na kujenga zahanati hii wakilalamika kwa kukosa huduma nyakati za usiku," anasema.

Mganga Mfawidhi huyo anasema changamoto iliyopo ni ukosefu wa mabenchi kwa ajili ya wagonjwa. Hivi sasa wanayo sita; mawili yanatumika na wagonjwa wa nje (OPD) na manne yanatumiwa na wajawazito wanaohudhuria kliniki na kuna wakati wagonjwa wanalazimika kuketi chini ya miti inayozunguka zahanati.

Anasema wanatarajia kutenga sehemu ya mapato ya zahanati, ili kuongeza mabenchi matano kwa ajili ya wajawazito na wagonjwa wa nje. Anasema wagonjwa kwa sasa ni wengi, wakiwa na wastani wa kuhudumia wajawazito 30 hadi 50 kwa mwezi, japo kuna miezi wanahudumia hadi wajawazito 80 kwa mwezi.

Shadia Abdully, mkazi wa kitongoji cha Njiapanda, anapongeza serikali kwa kusikia kilio chao cha muda mrefu na kupeleka nishati ya umeme kwenye zahanati waliyojenga kwa kuchangishana fedha.

Anasema waliokuwa wakipata adha hiyo ni wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano , kwa kuwa ndiyo kundi linalohitaji zaidi huduma za dharura usiku.

Mkazi wa kitongoji cha Ngoma, Ramadhani Ruzuba anasema kuwa mwaka jana, mkewe alijifungulia njiani na kuzalishwa na watu wasiokuwa na taaluma ya uuguzi wakati wakienda zahanati ya kijiji jirani kutokana na zanahati yao kukosa umeme.

John Nkwale, mlinzi wa zahanati hiyo anasema kuwa tangu zahanati ipate umeme, ameshuhudia wajawazito sita wa dharura wakipatiwa huduma usiku na muuguzi.

Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (2008), vinaelekeza serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya, kila wilaya iwe na hospitali ya wilaya na mkoa uwe na hospitali ya rufani ya mkoa. Pia vituo hivyo vya kutolea huduma viwe na miundombinu inayokidhi matakwa ya utoaji huduma za afya.



HABARI KITAIFA

# Ashikiliwa polisi tuhuma kumuua mtoto wa mwanakikundi mwenzake

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha linamshikilia Jaina Mchomvu, kwa tuhuma za kuhusika katika mauaji ya Mariam Juma (12), mkazi wa Kwa Mrombo, jijini.

Mwili wa mtoto huyo unadaiwa kukutwa na majeraha ya kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni na maeneo mbalimbali ya mwili wake na ulifichwa chini ya uvungu wa kitanda katika nyumba ya mtuhumiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Justine Masejo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi mchana, eneo la Kwa Mrombo.

"Mtoto huyu alikuwa ametumwa dukani toka asubuhi lakini hakurejea na ilipofika mchana, wazazi wake walianza kumtafuta maeneo mbalimbali baada ya kuingiwa na wasiwasi," alisema.

Masejo alisema hadi sasa wanawashikilia watu watatu, akiwamo Jaina ambaye ni mama mwenye nyumba ambako mwili wa mtoto huyo ulikutwa.

Alidai kuwa mara baada ya kutenda tukio hilo, mtuhumiwa huyo alikimbilia Mabogini, Moshi, mkoani Kilimanjaro ambako alijificha.

Kamanda huyo alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru), kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Akieleleza tukio hilo kwa kina, kamanda huyo alisema kuwa baada ya kukamatwa kwa mtuhumiwa Jaina, alihojiwa na kukiri kutenda tukio hilo la mauaji ya mtoto huyo.

Alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za kiuchunguzi, ili kubaini chanzo cha tukio hilo.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu na kutoa ushirikiano kuhusu wa tukio hilo.

Wakizungumza eneo la tukio, wakazi wa eneo hilo, akiwamo Juma Abdallah, walisema jirani yao alianza kumtafuta mwanawe kuanzia asubuhi, baada ya kumtuma vocha dukani bila kurudi.

"Lakini mchana alisikika mtoto mdogo kwenye nyumba inayodaiwa kumuua Mariamu, akisema ameona mkono kwenye beseni na watu tulipokwenda tukaona mtoto huyu amekatwakatwa na kuwekwa kwenye beseni lililowekwa uvunguji mwa kitanda cha huyu mtuhumiwa," alisema.

Alisema wakati huo mama mwenye hiyo nyumba hakuwapo, lakini alionekana majira ya saa tatu asubuhi, akipanga bidhaa kwenye genge lake.

Naima John alisema mtuhumiwa wa mauaji hayo ni mwanakikundi mwenzake cha mtaani cha kusaidiana, lakini hakuwahi kufikiria kama anaweza fanya unyama huo.

"Huyu mama aliamka asubuhi, akaenda sokoni kununua vitu vya gengeni, akapanga vizuri, lakini tukasikia kuna shida hii, watu wamekuta damu mlangoni kwake pakiwa pamedekiwa na kufagiliwa na tulipoingia ndani tukakuta mtoto huyu amechinjwa na kukatwakatwa na baadhi ya viungo na kuwekwa kwenye beseni," alisema.

Baada ya Polisi kuchukua mwili wa marehemu, Nipashe ilishuhudia wananchi wenye hasira kali wakibomoa nyumba hiyo na kuchukua vitu vyote vya ndani kila mmoja na chake.

Baadhi walichukua mabati ya nyumba hiyo, baada ya kuiangusha chini na wengine wakabeba matofali ya nyumba hiyo na kuacha eneo hilo likiwa jeupe.



**Mtoto huyu alikuwa ametumwa dukani toka asubuhi lakini hakurejea na ilipofika mchana, wazazi wake walianza kumtafuta maeneo mbalimbali baada ya kuingiwa na wasiwasi.**

Kamanda Justine Masejo


## TANGAZO LA MNADA

**Ayden, Rapitech, Marmboto, Freemind,Mofano,Rapitech,workethic na Josina** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Wa nyumba na magari Jijini Dar es saalam, Morogoro,Mwanza na Katoro Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Jina la Mteja | Aina ya Dhamana | Mji | Dalali | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ASUMITE SONGWE MUSOMBA | TOYOTA PICNIC T625 DFW | Dar es salaam | Ayden | 28.10.2024 |
| 2 | FAREED ISSA KONDO | Toyota NOAH T507CTX | Morogoro | MARMBOTO | 28.10.2024 |
| 3 | William Mathias Magina | Toyota STARLET,T583AKX | Dar es salaam | FREEMIND | 28.10.2024 |
| 4 | Greyson Fredrick Mateni | Toyota SPACIO T239 CJL | Dar es salaam | Mofano | 28.10.2024 |
| 5 | ALBERT RWAMUGIRA MUTALEMWA | Toyota STARLET T620 BAW | Dar es salaam | RAPITECH | 28.10.2024 |
| 6 | MOSES MLIGO MUSSA | Toyota ARISTO T929DJU | Dar es salaam | Work ethic | 28.10.2024 |
| 7 | Paul Joseph Msambila | Subaru IMPREZA SPORTS T445EEY | Dar es salaam | RAPITECH | 28.10.2024 |
| 8 | Zabron Abraham Mabwana | Kiwanja kipo Njegezi | Mwanza | JOSINA | 28.10.2024 |
| 9 | Ibrahim Kalazile Salum | Kiwanja kipo Kanyerere | Mwanza | JOSINA | 28.10.2024 |
| 10 | Patrick Faustine Magai | Nyumba ipo ILEMELA, NYASAKA B | Mwanza | JOSINA | 28.10.2024 |
| 11 | PAULINA WILFRED KISHER | Kiwanja kipo – BUHONGWA KASESE | Mwanza | JOSINA | 28.10.2024 |
| 12 | Joseline Christian Ferdinand | Kiwanja kipo Igoma | Mwanza | JOSINA | 28.10.2024 |
| 13 | Sylivester Rwebangira Laurian | Kiwanja kipo Ibondo Lumasa | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 14 | Judith Kailu Bajwaka | Kiwanja kipo Buziku | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 15 | Kayanda Willison Samike | Kiwanja kipo Njiapanda | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 16 | Merciana Lusatila Kazumulo | Nyumba ipo Lwamgasa | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 17 | William Elias Songoma | Nyumba Bugayambelele | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 18 | Frank Samwel Kanyoloku | Nyumba ipo Nyarututu | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |
| 19 | Esther Charles Masatu | Nyumba ipo Nyamigota | Katoro | JOSINA | 28.10.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa)**




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# DR Congo inafungika, Stars kazeni buti twende AFCON 2025

**KESHO** Jumanne Timu ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salam kuikaribisha Timu ya Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DR Congo), katika mchezo wa kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON 2025).

Mchezo huo ni wa Kundi H, ambalo mbali ya Tanzania na DR Congo pia zimo Ethiopia na Guinea ambazo zilicheza mechi yao ya raundi ya tatu juzi na wenyeji wa mechi hiyo, Waguinea wakashinda mabao 4-1.

Ushindi huo unaifanya Guinea kufikisha pointi tatu na kujiimarisha kwenye nafasi ya tatu nyuma Stars yenye alama nne, huku vinara wa kundi hilo wakiwa ni DR Congo yenye pointi tisa na Ethiopia ikiburuza mkia kwa alama yake moja.

Hivyo, ushindi wa aina yoyote kwa Taifa Stars kesho ni muhimu sana, ili kujiweka katika njia sahihi ya kufuzu kwa mara ya nne kushiriki fainali hizo zitakazofanyika baadaye mwakani nchini Morocco.

Hii ni baada ya kutoka sare mchezo wa kwanza nyumbani dhidi ya Ethiopia na kwenda kushinda ugenini dhidi ya Guinea, hivyo bado itakuwa na kibarua kigumu ugenini kwa Wahabeshi.

Mechi nyingine ambayo itakuwa ni muhimu pia kwa Taifa Stars ni pale itakapowakaribisha nyumbani Guinea.

Kama Stars itapambana na kushinda dhidi ya DR Congo kesho, itafikisha pointi saba ama ikishindikana na kuambulia angalau sare itakuwa na alama tano, hivyo kuzidi kuongeza pengo kubwa dhidi ya wapinzani wao Guinea.

Ikumbukwe katika kila kundi kati ya makundi 12, vinara wawili watafuzu kushiriki fainali hizo, hivyo mpaka sasa DR Congo inahitaji pointi moja tu kufuzu na kuacha mbio kubwa kwa Tanzania na Guinea kuwania nafasi moja itakayobakia kutoka katika Kundi H.

Kwa maana hiyo kinachotakiwa kwa Stars ni kushinda kesho, ili kupunguza kucheza kwa presha kubwa katika mechi zake mbili za mwisho hususan itakapokutana na Guinea ambao wanafukuzana kuwania nafasi hiyo moja.

Sisi kama wadau namba moja wa sekta ya michezo nchini, tunaamini inawezekana kwa Stars kushinda ama kupata sare kesho, kwa sababu hata mchezo wao uliopita dhidi ya DR Congo ilicheza vizuri na kama si bao la kujifunga la Clement Mzize, ingeweza kupata sare ugenini.

Lakini pia tunaamini benchi la ufundi chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco', litakuwa limeona panapovuja katika kikosi chao na kufahamu ubora na udhaifu wa wapinzani wao.

Kinachotakiwa kufanya sasa, kazi kubwa iliyobaki ni kwa wachezaji kuona umuhimu na thamani ya jezi ya taifa na kutambua wanawakilisha zaidi ya Watanzania milioni 60, hivyo waingie uwanjani kwa kazi moja ya kusaka ushindi.

Katika hilo pia, kwa kuwa mechi hiyo inachezwa nyumbani, kuna haja ya mashabiki kuitumia vyema nafasi ya kuwa mchezaji wa 12 kwa kujitokeza kwa wingi na kuujaza uwanja kesho.

Nipashe tunatamani kuona hatuishii kuujaza tu uwanja, bali wingi huo uende sambamba na kuishangilia Stars mwanzo mwisho bila kujali tumetanguliwa kufungwa ama la.

Mashabiki watakavyoishangilia kwa nguvu timu yao, itawongezea nguvu wachezaji na kujiona wanadeni la kuhakikisha ushindi unapatikana kwenye ardhi ya nyumbani ya Mama Samia Suluhu Hassan.

Hilo likifanyika vyema kama ambavyo hufanyika pale klabu zetu pendwa zinapokutana, tunaamini DR Congo wataziacha alama tatu.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mkakati kuzalisha mastraika, viungo bora watakiwa nchini

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya mchezo kati ya Taifa Stars na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, nilimsikia Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco,' akibainisha wazi tatizo lililopo katika kikosi chake ni ushambuliaji na kutengeneza nafasi.

Stars itashuka tena dimbani kesho kuwavaa DR Congo katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

"Sehemu ambayo naiangalia zaidi ni ushambuliaji, inabidi tunoe safu yetu, pia tunatengeneza nafasi chache sana, inabidi tufanye kazi hiyo, kufanya viungo wetu watengeneze nafasi ya mastraika wazitumie kwa ufasaha," alisema Morocco.

Hii ni baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Alhamisi iliyopita, huku Stars, iliyokuwa ugenini kupoteza kwa bao 1-0.

Kwa matokeo yoyote yatakayopatikana kesho, lakini alichokisema Morocco ndicho kwa sasa kinaakisi soka letu nchini.

Tanzania kwa sasa haizalishi na wala haina vipaji vya mastraika na viungo washambuliaji wenye jicho zuri la pasi za mwisho, au kutengeneza makosa kwa mabeki kiasi cha kuachia mianya.

Kwa sasa nchi yetu imejaaliwa viungo wakabaji wengi wazuri, ndiyo maana tunamwona Mzamiru Yassin, Yusuph Kagoma, Novatus Dismas, Baraka Majogolo, Himid Mao, Kelvin Nashon, Aziz Andambwile na wengineo.

Ukiangalia hapo kwa sasa hata wachezaji wetu wanaopata nafasi ya kusajiliwa nje ya nchi wengi wao wanacheza nafasi hiyo, kama Himid, anayekipigaTala'ea El Gaish ya Misri, Novatus anayeitumikia Goztepe ya Uturuki na Majogolo ambaye kwa sasa yupo Chippa United ya Afrika Kusini.

Hii tu peke yake inaonyesha kwa sasa Tanzania inazalisha viungo wakabaji wengi. Ingawa si vibaya, lakini inatakiwa pia mkakati ufanywe ili kutengeneza au kusaka vipaji vya wachezaji ambao ni mastraika na viungo washambuliaji.

Klabu hazina tatizo sana kwa sababu zenyewe zina uwanda mpana na kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi ambao wamekuwa wakifanya vyema.

Tumewaona wachezaji kama Stephane Aziz Ki, Clatous Chama, Pacome Zouzoua, Jean Charls Ahoua ambao ni baadhi ya viungo washambuliaji wenye uwezo mkubwa wa kutoa pasi za mwisho za upendo wakiwa na timu zao.

Wachezaji wa aina hii hawapo kwenye kikosi cha Stars kwa miaka ya hivi karibuni tofauti na zamani ambapo kulikuwa na kina Athumani China, Issa Athumani, Hussein Masha, Dan Mhoja, Shekhan Rashid, Hamisi Gaga 'Gagarino', ambao walikuwa na uwezo mkubwa na kusimama kati na kutengeneza mabao kwa washambuliaji.

Nchi ina uhaba wa mastraika kwa sababu tangu alipopatikana, Mbwana Samatta aliyeanza kucheza soka la ushindani mwaka 2008 akiwa na African Lyon, kabla ya kujiunga na Simba 2010, pamoja na mwenzake, John Bocco ambaye kila msimu alihakikisha anafunga mabao zaidi ya 10, hadi sasa hajapatikana straika wa maana anayeweza kuvaa viatu vyao.

Mastraika wengi wa kitanzania, huibuka msimu mmoja na kuyeyuka kama kipande cha samli juani, ubora unakosekana na wengi wao ni wale ambao kwa msimu mzima anafunga mabao matano au sita.

Miaka ya 1970 na 1980, nchi hii ilibarikiwa mastraika hatari waliotapakaa kila timu nchini kama Zamoyoni Mogella, Peter Tino, Mohamed Hussein 'Mmachinga', Abeid Mziba, Malota Soma, Makumbi Juma, Abdallah Buruhani, Ally Katolila, Hamza Mponda, Kitwana Selemani, Jimmy Mored, Cheche Kagile, Mohamed Chopa, John Makelele 'Zigzag', Edward Chumila, Mohamed Mgalike, Emmanuel Tenende, Zuberi Magoa, na wengine wengi kiasi hata iliwapa tabu makocha wa Stars kuteua.

Nadhani kuna sehemu tumekosea. Inawezekana vipaji vimepungua kutokana na sababu mbalimbali za kibaiolojia, lakini unaweza kufanyika mkakati wa kuwatengeneza mastraika hata wa kufundishwa.

Nikisema hivi sina maana tuwapunguze mastraika kwenye timu za Ligi Kuu, hapana, ni kuleta au kuandaa makocha ambao watakuwa na mpango mkakati wa kusaka vipaji hivyo kuwatengeneza, ili baada ya miaka mingi kupita zirejee zile enzi la mastraika Watanzania walitetemesha Afrika Mashariki na Kati.

## HABARI KITAIFA




Makamu wa Rais Afrika Mashariki Iqbal Ahmed, akizungumza katika kongamano la madaktari Bingwa na Wamiliki wa hospitali lililofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, kuhusu huduma zinazotolewa na maabara za Metropolis yenye makao yake nchini India. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Metropolis kushirikiana na serikali, sekta binafsi uchunguzi kimaabara

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Metropolis inayojihusisha na huduma za uchunguzi wa kimaabara imesema iko tayari kushirikiana na taasisi za afya za serikali na binafsi, ili kuziba pengo la maabara Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuzisogeza karibu na wananchi.

Mtaalamu wa Patholojia na Kiongozi wa Operesheni za Kiufundi kutoka Metropolis, Dk. Rameez Patvegar, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki walipokutana na madaktari, wafanyakazi wa maabara na wamiliki wa hospitali kuwaeleza huduma wanazotoa.

Katika mkutano huo, Dk. Patvegar alieleza namna Metropolis wanavyotumia teknolojia mpya ambazo huongeza uwezo wao wa kutoa matokeo sahihi ya kimaabara.

Alisema kuna haja kwa sekta ya afya nchini kutumia maabara za uchunguzi za Metropolis na kushirikiana kila inapowezekana kwa lengo la kupanua haraka huduma hiyo muhimu katika mikoa mbalimbali.

Dk. Patvegar alisema wanahamasisha Tanzania kutumia maabara ya Metropolis kwa sababu ndiyo pekee inayotoa vipimo zaidi ya 3,000 vyenye utaalamu wote maalum kwa magonjwa ya saratani, mzio na yanayohusiana na vinasaba.

"Tumewekeza sana kwenye ubora. Si tu majaribio hata ubora. Ripoti zetu ni sahihi sana na ni kwa gharama nafuu. Kwanini Tanzania? Kwa sababu tunaona kuna pengo kubwa la huduma ya afya.

"Tuko tayari kushirikiana na taasisi zote za serikali na sekta binafsi ili kuziba pengo la huduma ya afya Tanzania na Zanzibar," alisema.

Dk. Patvegar alisema kuwa India wamewekeza katika sekta ya umma na kuomba wadau na serikali kuwaunga mkono kwa sababu wanalenga ubora kulingana na viwango vya kimataifa vinavyotaka.

"Maabara zetu nyingi ambazo zinapatikana kote ulimwenguni, zina kibali na zinafuata viwango sawa. Tuna mtandao mpana, hutuwezesha kutoa huduma bora zaidi kulinganishwa na maabara zingine.

"Maabara nyingi zinakosa upatikanaji huu wa huduma kwa sababu ya mtandao mdogo au kwa sababu ya utaalamu mdogo. Tuna utaalamu bora zaidi. Tuna madaktari 200 ambao hutoa matokeo na ripoti bora. Dar es Salaam tuna maabara tatu," alisema.

Aliongeza kuwa walikutana na wadau hao kuwaeleza wanayofanya kazi na teknolojia mpya walizonazo na namna zinavyowezesha kutoa matokeo sahihi.

Kiongozi wa kampuni hiyo nchini, Imtiaz Shaikh, alisema hadi sasa wako katika nchi saba na wana matawi zaidi ya 70 na mpango walionao ni kuwa na matawi mengine 50.

Shaikh alisisitiza umuhimu wa Watanzania kujiunga katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za huduma za afya.

"Kati ya wanaotafuta huduma, ni wachache sana wameandikishwa katika bima ya afya. Ni muhimu kwamba tutetee watu wetu kujiandikisha na NHIF, ili kuhakikisha upatikanaji huduma muhimu za afya kwao," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia mipango hiyo, Metropolis inalenga si tu kuimarisha huduma za maabara bali pia kuchangia ipasavyo katika huduma za afya Tanzania Bara na Zanzibar katika kuboresha huduma kwa wananchi.


**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Wizara ya Uchukuzi**
**Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania**

# TANGAZO

## TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA KWA AJILI YA MRADI WA USANIFU NA UJENZI BANDARI YA KISIWA/MGAO, WILAYA YA MTWARA, MKOA WA MTWARA.

Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ina jukumu la kusimamia shughuli za bandari zote zilizopo ndani na pembezoni mwa mipaka ya Tanzania. Akiwa kama mmiliki na mwendeshaji wa bandari hizi, baadhi ya majukumu ya TPA ni pamoja na kutangaza, kuendeleza na kusimamia shughuli za uendeshaji wa bandari pamoja na maeneo yanayozunguka. Mamlaka ya Bandari pia ina jukumu la kuingia mikataba mbalimbali inayohusiana na uendeshaji wa bandari kwa niaba ya serikali. TPA inasimamia uendeshaji wa bandari kadhaa za baharini pamoja na bandari zilizomo kwenye maziwa ya Tanzania zikiwemo bandari kubwa za za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Bandari imeazimia kutekeleza ujenzi wa bandari ya kusafirisha mizigo maalumu kama makaa ya mawe, saruji, chuma itakayojengwa mpakani mwa vijiji vya Kisiwa na Mgao. Dhumuni kuu la mradi huu ni kuongeza tija na ufanisi wa shughuli za usafirishaji katika ukanda wa maendelo wa Mtwara.

Ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, TPA, kupitia kampuni iliyoshinda kandarasi ya kusanifu na kujenga bandari ya Kisiwa/Mgao imeipatia Eco Services (T) Limited, ambayo ni kampuni ya washauri waelekezi wa mazingira kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya shughuli za ujenzi wa bandari kuanza. Mchakato wa tathmini ya athari za mazingiria utasaidia kupata maoni ya wadau wataokaoathirika na mradi pamoja na mapendekezo ya hatua stahiki za kukabiliana na athari zinazoweza kusababishwa na mradi. Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 31 Oktoba 2024.

Endapo una maoni au maswali kuhusu mradi huu, unaweza kuyatoa au kuyatuma katika ofisi zifuatazo ambapo taarifa zaidi za mradi zinapatikana;

| | |
|---|---|
| **Mwendelezaji** | Mkurugenzi Mkuu,<br>Mamlaka ya Bandari Tanzania<br>S. L. P. 9184, Dar es salaam, Tanzania<br>Simu: 0800-1100 32<br>Faksi: +255 22 2130390<br>Barua Pepe: dg@ports.go.tz Tovuti: www.ports.go.tz |
| **Mshauri Mwelekezi wa Mazingira** | Mkurugenzi Mtendaji<br>Eco Services (T) Limited,<br>Regent Estate, Kiwanja Na. 132/2, Mtaa wa Migombani<br>S. L. P. 36086, Dar es Salaam, Tanzania<br>Simu: +255 787 696 932<br>Barua Pepe:info@ecoservices.co.tz Tovuti:www.ecoservices.co.tz |
| **Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)** | Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)<br>Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 6<br>S. L. P. 2724 Dodoma, Tanzania<br>Simu: +255 26 2960098, 0713608930<br>Barua Pepe: dg@nemc.or.tz Tovuti:www.nemc.or.tz |

# Zungu ataka uwekezaji teknolojia mpya ya miwa

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

NAIBU Spika wa Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Ilala, Mussa Zungu, amewataka wadau wa sekta ya sukari kuwekeza katika teknolojia ya kisasa na ubunifu, ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wilayani Kilombero, mkoani Morogoro wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakulima wa Miwa Bonde la Kilombero, iliyokwenda sambamba na maonesho ya siku tatu ambapo wakulima wa miwa walipata fursa ya kuwasiliana na wadau wengine ndani ya sekta hiyo na hivyo kuendelea kupata mawazo mapya yatakayoendelea kukuza uzalishaji wao.

Maonesho yalijumuisha vifaa mbalimbali vya kilimo, mbegu bora, matumizi sahihi ya mbolea na mbinu mbalimbali za kudhibiti magonjwa na wadudu katika zao la miwa.

Zungu aliwataka wakulima na wadau wengine kuwekeza katika kupata teknolojia mpya na ubunifu, ili kuboresha mavuno yao, kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kujiletea maendeleo.

"Mada ya mwaka huu ni kuwawezesha wakulima wa miwa kupitia teknolojia na uvumbuzi, njia ya kuongeza tija na utoshelevu wa sukari na ndio maana ninatoa wito kwa wakulima na wadau kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika maeneo hayo, kwa kuwa ndiyo njia pekee itakayoongeza uzalishaji.

Zungu pia alipongeza mradi unaoendelea wa upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero na kuhimiza jitihada zinazoendelea za kuongeza upatikanaji sukari, ili kuwezesha nchi kujitegemea kwa sukari.

"Nimefurahishwa na maendeleo yaliyopatikana kwenye mradi wa upanuzi. Ninaomba kampuni iongeze juhudi, ili kuziba upungufu unaosababishwa na maendeleo ya pole pole wakati wa mvua.

Akizungumzia upanuzi wa kiwanda cha K4 ambacho ujenzi wake umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni ya sukari Kilombero, Derick Stanley, alisema upanuzi huo utakapokamilika utaongeza maradufu uwezo wa kampuni hiyo wa kusindika sukari kwa kuzalisha tani 144,000 za ziada kwa kila mwaka.

Kiwanda hicho kipya pia kitakuwa na zaidi ya mara mbili ya miwa inayopatikana kutoka kwa wakulima. Lengo letu ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha inajitosheleza kwa sukari kupitia sukari inayozalishwa nchini.

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SINGIDA (SUWASA)

MIAKA 25 YA KUMBUKIZI YA
BABA WA TAIFA
MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE
1999 - 2024



Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi na Watumishi wote wa SUWASA wanaungana na Watanzania wote katika Maadhimisho ya kumbukizi ya Baba Wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere

#Sekta ya Maji tumepiga hatua

suwasa_singida | Suwasa Singida | Bure 0800710038 | www.suwasa.go.tz

# TAMWA, TCRA kutoa tuzo kwa waandishi wa habari za maendeleo

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), wanatarajia kutoa tuzo kwa waandishi wa habari na maofisa habari wa serikali waliochapisha maudhui yanazohusu maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi.

Tuzo hizo zinalenga kuchochea uandishi wa makala zilizofanyiwa utafiti na uchambuzi kuhusu maendeleo, uwajibikaji, uzalendo na kujenga chapa na taswira ya nchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa tuzo hizo zinazoitwa Samia Kalamu Awards, jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema zinatarajiwa kutolewa Novemba mwaka huu.

Alisema tuzo hizo zitahusisha maudhui yaliyochapishwa kupitia magazeti, redio, luninga na majukwaa ya mtandaoni yanayohusu maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi na fursa zinazopatikana kwenye miradi mbalimbali.

Alisema tuzo hizo pia zinalenga kuhamasisha wanahabari kuchapisha maudhui ya kuelimisha, kwa kuwa hivi sasa habari hizo zinaandikwa kwa kiwango kidogo.

"Kutokana na maendeleo ya teknolojia na utandawazi, uandishi wa habari nchini umekuwa ukijikita katika kuburudisha na kuhabarisha huku uandishi wa makala za kuelimisha ukiwa kwa kiwango kidogo," alisema.

Dk. Rose alisema tuzo hizo ni mwendelezo wa mafunzo ambayo taasisi hizo mbili zilitoa kwa waandishi wa habari, watangazaji, wahariri, mameneja, maofisa habari, wamiliki wa vyombo vya habari, wahadhiri na watengeneza maudhui ya mitandaoni 2,054 nchini kwa miezi mitatu.

"Pamoja na mafunzo yaliyotolewa, tuliona ni vyema kutoa tuzo kwa wanahabari pamoja na vyombo vya habari ambao wamekuwa wanafanya jitihada za kuandika, kuchapisha na kutangaza maudhui ya ndani hasa makala zilizofanyiwa utafiti na uchambuzi wenye tija kwa Watanzania," alisema Dk. Rose.

Alisema tuzo hizo zimepewa jina la Samia Kalamu Awards, ili kutambua na kuenzi historia ya kuwa Rais wa kwanza mwanamke nchini.

Aliwasisitiza wanahabari kuhakikisha habari watakazozishindanisha ziwe zimeandikwa kati ya Januari Mosi hadi Oktoba 26 mwaka huu.

Meneja wa Huduma za Mawasiliano wa TCRA, Andrew Kisaka, alisema ni matarajio yale kuwa tuzo hizo zitaleta matokeo chanya katika jamii na tasnia ya habari.

Alisema kupitia tuzo hizo, watafahamu uandishi wa habari zinazochochea maendeleo upo kwa kiwango gani na nini kifanyike, ili kuhakikisha maudhui yanaandikwa kwa kiwango cha hali ya juu na kukidhi viwango vya kimataifa.

Alisema waliamua kutoa mafunzo kwa wanahabari baada ya utafiti waliofanya kugundua kuwa waandishi wengi hasa wa luninga wanachapisha maudhui ya kuhabarisha na kuburudisha na kusahau kuchapisha makala za uchunguzi wa kina za maendeleo ya nchi.

Alisema katika mafunzo hayo walifundisha kuhusu uzalendo, utii na mbinu za uandishi wa habari wa kisasa unaoendana na maendeleo ya teknolojia.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA)
"HUDUMA BORA KWA FURSA ZA MAENDELEO"

MIAKA 25 YA KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE



25 MIAKA
1999 - 2024

Bodi ya Ushauri, Menejimenti na Watumishi wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na wananchi wote kuadhimisha miaka 25 ya kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. TEMESA tutaendelea kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma bora kwa fursa za maendeleo.


*Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA),*

Julius Kambarage Nyerere
(14/10/1999 - 14/10/2024)

TEMESA HOUSE
2 Mtaa wa TEMESA
41104 Tambukareli,
S.L.P 1075, DODOMA.

Namba za Simu: +255-737962496
Namba ya Bure: 0800110379
Barua Pepe :barua@temesa.go.tz

Tovuti :www.temesa.go.tz



# MIAKA 25 BILA YA NYERERE

Nipashe



# Malecela: Sitosahau ile siku alinituma kumwona Amin, niliona maisha rehani

• Alinichukua katika gari bila ulinzi, akaniendesha mitaa Kampala...

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NI majira ya saa 10 jioni ya Alhamis wiki iliyopita, nipo nyumbani kwake Mtaa wa Kilimani jijini Dodoma, mbele yangu yupo Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela mwenye umri wa miaka 90.

Mguuni ana viatu vya vijana 'raba', shati la kitenge, akiwa ametoka shambani kwake Chinangali, wilayani Chamwino wastani wa kilometa 30.

Anatukaribisha kwa kauli: "Samahani sana nimechelewa kurudi kutoka shambani, ili tufanye mahojiano, kama ambavyo mliomba. Ilikuwa muhimu kwenda kule shambani.

"Nilikwenda asubuhi, ili niwahi kurudi, maana katika shamba letu la ushirika leo tulikuwa tunakutana na Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ushirika. Karibuni sana ofisini kwangu," Mzee Malecela anatamka kwa bashasha la ukarimu.

Baada ya hapo anaketi, kisha anamaka kijasiri anatoka nje akisema: "Kabla ya kuanza mazungumzo yetu, ngoja nifuatilie kwanza soda, ili mlainishe makoo yenu. (alimuita Msaidizi wake) nileteeni soda na maji kwa ajili ya wageni wangu au 'can you have a glass of wine? (mnaweza kupata kinywaji mvinyo?)"

Alipojibiwa kuwa soda inatosha, anarejesha masihara yaliyobeba maana kwa mwanahabari mpiga picha (Peter Mkwavila): "Umemuona Yesu? Lakini nitakupa kitabu kimoja utakisoma siku nyingine....

"Kimeandikwa na Myahudi anasema hivi nyie dunia nzima mna ugonjwa gani? ....Huyu mwandishi ameandika historia fupi ya 'humankind' wanadamu walitoka wapi? Anasema wataalamu wote duniani wanakubaliana kwamba mtu wa kwanza alitoka Olduvai Gorge..."

Hapo ndipo anaanza simulizi yake, alivyomfahamu Nyerere kwa karibu, akisema mambo makuu kadhaa.

Mosi, anasema alikuwa mnyenyekevu, mwenye huruma, upendo, unyenyekevu na mtiifu., akiendelea: "Mwalimu Nyerere wakati mwingine alikuwa anaweza kuvaa shati bila vesti.

"Alikuwa mnyenyekevu, mtiifu, anayependa watu. Nikupe mfano mmoja tulikwenda Canada sasa tukiwa pale jioni kulikuwa na TV (runinga), kwa hiyo mimi nikaenda nikaifungua.



Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela alipozungumza na Nipasahe nyumbnani kwake Alhamisi, wiki iliyipoita nyumbani kwake jijini Dodoma. **PICHA NA PETER MKWAVILA**

"Baada ya kufungua kulikuwa na ngumi wakati huo, alikuwa anampiga mwenzake sana, Mwalimu akasema 'John, John zima! hiyo kwanini mnaangalia vitu vya kikatili namna hiyo...', 'so that was' (huyo alikuwa) Mwalimu," anasema.

Anasema usomi wa Mwalimu Nyerere, pamoja na kuwa mtu mwenye akili sana, ilimsaidia kuwa mtu wa aina hiyo.

"Alisoma chuo kikuu kilichopo Scotland, nadhani kilimsaidia sana, acha tu alikuwa na akili za kuzaliwa, lakini pia za kunolewa zilichanganyika zikafanya kitu kizuri. Kwa hiyo Mwalimu alikuwa mtu mwenye huruma sana, vitu vyote alikuwa anaangalia hivyo," anasema.

Pili, anasema Mwalimu Nyerere alikuwa anapenda sana familia yake na katika matumizi ya fedha alikuwa si mtu wa matumizi mabaya kuanzia kuvaa kwake.

"Katika kuvaa kwake nadhani Watanzania wote watakubaliana na mimi, ni mara chache ulimkuta Mwalimu amevaa tai, 'otherwise' Vinginevyo, alikuwa akivaa 'duara' yake (mashati ya Chuo En lai).

"Ile, Mwalimu alikuwa anapenda sana familia yake lakini lazima nikubali mara nyingine madaraka ya nchi yalimfanya ayashughulikie mno kushinda wajibu wake kwa familia," anaeleza.

"Mimi nafikiri kuna wakati watoto wa Mwalimu walitaka mapenzi ya baba yao, lakini hawakupata ya kutosha, kutokana na majukumu ya kitaifa aliyokuwa nayo Mwalimu," anasema.

Anabainisha, alikuwa mtu mwenye malengo na kwamba alipokwenda Umoja wa Mataifa, alionesha kwanini anataka uhuru wa Afrika.

"Desemba 12, 1962 alisema kwenye Umoja wa Mataifa kwamba, Tanzania hatuwezi kufurahia uhuru wetu kikamilifu hadi Bara la Afrika liwe huru. Uhuru wa Afrika kwa asilimia kubwa ilikuwa ni nguvu ya Mwalimu.

"Mwaka 1963 OAU ilipozaliwa, Mwalimu alikwenda Addis Ababa kuhudhuria kuzaliwa kwa OAU na ndipo alikwenda kuweka azimio OAU tusikubali uhuru wa nchi zetu umekamilika hadi Bara zima la Afrika liwe huru.

"Na hapo ndipo likapitishwa azimio la kuunda Kamati ya Ukombozi ya Bara la Afrika, Mwalimu akasema tukiunda makao makuu yaleteni kwangu, ndio maana yakawa Tanzania," anasimulia.

Hapo anarejea kumbukumbu, Mkuu wa kwanza wa kamati hiyo, alikokuwa ni Sebastian Chale kutoka Songea na baadae akaja George Magombe na Hashim Mbita, alikuwa wa mwisho.

"Kamati hii Mwalimu alitaka Tanzania tuitumie kama blanketi na ilikuwa viongozi wa Afrika wakikaa wakisema uhuru wa Afrika na kwamba watakavyosaidia mapinduzi, mtu anasema kabisa anatokwa hadi na jasho.

"Lakini ukiwaambia kulipa kwenye kamati hawawezi, wanasema maneno makali, sisi Tanzania tunasema sawa, sasa sisi hapo hapo ndio tunajificha na ukali wote tunaupeleka kuwa Bara la Afrika linasema na ilitusaidia sana," anasimulia.

Anakumbuka Samora (Machel) alivyomfuata Mwalimu Nyerere akimwambia kuna watu wake porini anaomba kwa njia yoyote apelekewe magunia 10,000 ya mahindi na iliwezekana kimya kimya ndani ya wiki mbili.

### AONANA NA AMIN

Anaisimulia Nipashe, kitu ambacho hatokisahau kwa kiongozi huyo (Mwalimu Nyerere) ni wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, alimtuma kwenda kukutana na Idi Amini, kujaribu kupata suluhu kuwaokoa wanafunzi wa Kitanzania katika Chuo Kikuu cha Makerere na Chuo cha Mafunzo ya Urubani cha Soroti, Uganda, ambao walikuwa wamewekwa kizuizini na kuwapo tishio la kuuawa.

"Kutokana na habari za siri, tulisikia Amin anataka kuwakamata wale watoto awe anawachinja kwa ajili ya kumtishia Nyerere. Hivyo hivyo, tukawa na hakika kama hatutafanya njia ya kuwaokoa watachinjwa.

"Mwalimu akaniambia, lazima uende na uhakikishe wanafunzi wetu wanatoka salama," anasema na jukumu, alilokuwa amepewa ni kuomba Amin awaachie wanafunzi waliokuwa wanashikiliwa.

Kwa mujibu wa Malecela, uamuzi wa kwenda Uganda kuonana na Amin ulitaka ujasiri na aliweka rehani maisha, yake kwa kuwa Amin alikuwa mtu ambaye angeweza kufanya lolote na wakati wowote, bila kujali wala kuhofia chochote.

Anasimulia katika mazungumzo yao na Amin, alimtamkia Tanzania chini ya Mwalimu Nyerere, ilikuwa inapingana na utawala wake, lakini Malecela akamjibu 'serikali ya Tanzania haikuwa na tatizo naye kabisa.'

Kutokana na jibu hilo, Amin aliagiza apelekewe gari ili amwendeshe Malecela mitaa mbalimbali ya Kampala. Hapo Malecela. Anasimulia: "Gari aliloletewa Amin alipoliwasha halikuwaka.

"Ikabidi iletwe jingine haraka na Amin inaendesha nikiwa nimeketi upande wa abiria. Tupo wawili tu, hatukuwa na ulinzi alitaka kunionyesha jinsi anavyopendwa Uganda.

"Tulipofika sokoni Nakasero Kampala, Amin aliegesha gari na watu walipomwona walianza kumshangilia. Amin, akanitambulisha akasema: "Mmeona? Mimi sina tatizo na Nyerere wala Tanzania. Huyu hapa ni Waziri wa Nyerere, amekuja kututembelea.

"Na mimi nimemleta mumuone muone sina tatizo na Nyerere. Kuanzia leo nisisikie Mtanzania yeyote anasumbuliwa hapa Uganda. Sisi na Wtanzania ni ndugu."

Anasema walipotoka sokoni, walizunguka maeneo mengine ambayo Amin aliendelea kumtambulisha Malecela na kusisitiza undugu wa Tanzania na Uganda.

"Wakati anafanya mazungumzo na Amin, upande wa pili kulikuwa na operesheni ya kuwatorosha wanafunzi waliokuwa wanasoma Makerere na Soroti.

"Wale wa Makerere wote walirejeshwa Tanzania salama. Shida ilikuwa kwa wale wa Soroti walikuwa 21 wao walisema wasingeondoka, kwa sababu

INAENDELEA UK. 10.

# Malecela: Sitosahau ile siku alinituma

INAtoka UK. 9.

walibakiza mwezi mmoja ili kufanya mitihani yao ya mwisho ya kumaliza masomo ya urubani," anasema.

Soroti ni chuo kichotoa mafunzo ya urubani na watalaamu wengi wa Afrika Mashariki walisoma huko.

Anasema aliporejea Tanzania na baada ya kubainika wanafunzi wa Kitanzania waliokuwa Makerere 400 tayari walishatoroshwa, wale 21 wa Soroti wote waliuawa na askari wa Amin.

**NYERERE NA KAWAWA**

Anasimulia Mwalimu Nyerere alikuwa mwanasiasa na Watanzania walimuelewa, lakini wakati kulikuwapo propaganda za kuigawa nchi kidini na vilizuka vyama vitatu (zama za kugombea uhuru).

"Kama Watanzania tusingekuwa makini tungegawanyika, sasa wakati huo Kawawa alikuwa mtu wa chama cha wafanyakazi (TFL), mtu wa kuitisha migomo ya wafanyakazi na alikuwa vizuri.

"Ili tusiingie kwenye migawanyiko ya kidini Kawawa aliiona hiyo na Nyerere akaiona wakawa pamoja kwa hiyo vyama vya wafanyakazi vyote vikawa wao na TANU ni kitu kimoja," anasema.

Anafafanua Kawawa, alipoungana na Nyerere, alikuwa na nguvu ya wafanyakazi (chama cha TFL) na walifanya kazi kwa ushirikiano mkubwa.

"Lazima nikubali kitu kimoja, Kawawa akawa ni mtu anayeheshimu usomi wa Nyerere na ujuzi wa Nyerere. Walipoungana na walivyofanya, ndio hadi sasa Tanzania tupo tulipo na Tanzania ya leo ukitaka watu wakuchukie kweli kweli sema habari ya dini,"anasema.

**SIRI YA MAAZIMIO**

Anasema Mwalimu Nyerere, kila kitu alichotaka kuanzisha kipya alianzia kwenye chama kujadili na kuja na kitu kama kwenye Azimio la Arusha, Azimio la Iringa (Siasa ni Kilimo), Azimio la Musoma (Elimu) yenye kuwapa Watanzania matumaini.

"Azimio la Arusha liliitisha watu na alikwenda kufanya kwenye 'kakibanda' kadogo na wengi walifikiri tukifika pale tutashindwa, kwamba tutapata migomo watu wataandamana, walidhani ni mwisho wa TANU.

"Lakini kilipotokea mabenki kutaifishwa mimi niliona watu wa serikali wanaingia NBC, watu wapo nje tu wanafurahia eeehe eehee! na ilikuwa kila sehemu matawi yalipo,"anasema.

Anafafanua kuwa baada ya Arusha, likaja Azimio la Iringa na lilizalisha suala la 'Siasa ni Kilimo' na wakulima majeuri walikuwa Iringa na Mbeya.

"Azimio lilitaka kuonyesha Watanzania wafanye nini kwenye kilimo. Lilizungumzia 'aspects' za mazao kwamba yalimwe na wapi na masoko yake yawe wapi. Mwalimu alitaka kuwaondoa Watanzania kwenye mawazo ya siasa na alitaka kuwapeleka kwenye kilimo," anasema.

Mzee Malecela anasema baada ya azimio hilo, alikuja na linalohusu elimu na lilifanyika Musoma, akiendelea: "Mambo mengi yanayotekelezwa sasa ni ya Azimio la Musoma la Elimu, kwa kweli utaona miongozo ya namna ya kujenga Tanzania bora na inayojali maskini inatokana na chama tawala," anasema.

**OPERESHENI VIJIJI**

Anasimulia siasa za Tanzania zinatokana na miongozo iliyotokana na Mwalimu Nyerere kwa kila sekta kama elimu, kilimo na afya, pia ana ufafanuzi wake:

"Kikubwa alichofanya Mwalimu Nyerere kukumbukwa ni alipokuwa anaendesha Operesheni Vijiji vya Ujamaa, alikuwa Chamwino kwenye 'mbuyu wake' bado upo na kivuli chake...alikuwa anasema hivi 'John (Malecela) kapeti likiwa chini unaliona zuri, hebu liinue ndani utakuta uchafu mwingi.

"Akasema vijiji vyetu tuvirundike pamoja, watu waliokuwa wanapinga vijiji vya ujamaa na watu walikuwa wametawanyika lakini vilipoanzishwa vijiji ikawa rahisi kushirikishana shughuli za kijamii.

"Wapinzani wakaidaka wakasema ooho watu wanakufa, kwa kweli tulipofanya vijiji tulilifungua kapeti ili tuondoe taka za chini,"anasema. Anabainisha kwenye vijiji wamepeleka zahanati, shule za msingi, maji safi na hayo yote yametokana na siasa ya operesheni vijiji.

"Mawazo ya Mwalimu hadi leo bado ni mwongozo na mimi nitasikitika sana kama tutafika mahali tusichukue mawazo ya Mwalimu ni msingi wa maendeleo Tanzania," anasema.

**DODOMA MAKAO MAKUU**

Anasema Mwalimu Nyerere alipokuja na Azimio la Kuhamia Dodoma, lililetwa na Paul Bomani, kwa kauli: "Watu wa Mwanza tunatoka mwisho wa reli hadi mwisho, Mwanza hadi Dar es Salaam.

"Kwanini tusitafute makao makuu mahali kwamba wenzetu wa Dar es salaam watakuja na sisi wa Mwanza tutakuja ndio ikawa Dodoma." anasema.

Anabainisha Mwalimu Nyerere hakushindwa kuwezesha kuhamia Dodoma, lakini wakati akiwa katika mkakati huo ndio nchi ikakumbwa na vita vya Idd Amin na ilichukua uchumi kwa kiasi kikubwa.

***• Kesho, fuatilia maisha yake Mzee Malecela, alikotokea na mengi aliyofanya kufikia leo, umri miaka 90.***

KUTOKA SHULE KONGWE NCHINI...

# Mwalimu wake amwibukia na kituko, Nyerere akamridhia kwa unyeyekevu

**• Mahali walikopatikana wanne waliomfundisha**

**Na Cheji Bakari**

WAKATI leo nchi inaadhimisha miaka 25 tangu kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipofariki dunia, Oktoba 14 mwaka 1999, wilaya ya Muheza inajivuna kuwa na shule nne mzizi wa walimu waliomfunza mwasisi huyo wa taifa.

Mahali hapo Muheza, hivi karibuni kulikuwapo na tamasha la 'Juma la Elimu,' ambalo limekwenda sambamba na uchangiaji vifaa vya elimu na uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha elimu inayoitwa "Mtoto wa Leo, Samia wa Kesho".

Ni tukio lilioandaliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Zainabu Abdallah, pia mbunge wa jimbo hilo, Hamis Mwinjuma - Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, mgeni rasmi mwalikwa, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

Dhana kuu katika tukio hilo, ilikuwa na historia ya chimbuko la elimu rasmi Tanganyika, chini ya utawala wa kikoloni, ikimgusa moja kwa moja Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere.

Hapo Dk. Biteko akasisitiza umuhimu wa elimu katika maendeleo ya taifa na kuzalisha viongozi bora kihistoria, kuwapo waliomfundisha Mwalimu Nyerere, kutoka shule hiyo inayosadikiwa kuwa ya kwanza nchini, iliyojengwa Muheza mwaka 1867, kijijini Magila.

Wakati inaanza chini ya muasisi, Padri Fraser kutoka Zanzibar, wanafunzi wake wanatajwa ni pamoja na; Jumbe Kifungiwe na ndugu yake Sagosago, pia vijana wengine Yustus Kazi, Steven Mhando, David Semfuko na Galo, wote wakawa walimu wa Mwalimu Nyerere.



Shule ya Magila, Muheza katika mwonekano wa sasa, ambayo inatajwa kuwa ya kwanza nchini, na walikosoma walimu wanne waliomfundisha Rais Julius Nyerere.

Kurejea andiko la kitabu chake, Luteni Kanali Mstaafu John Mhina, mkazi na aliyekwishakuwa mbunge wa Muheza 1990-95, wanafunzi waliohitimu shuleni hapo walikuwa fasaha katika lugha ya kiingereza na wachambuzi wa mahiri wa kitaaluma, hata kihistoria inatajwa, ufasaha kitaaluma wa Nyerere, unaoanishwa nao kutoka chimbuko la shule hiyo ya Wamisionari wa UMCA na Anglikana.

Inaelezwa, mbali na Nyerere, wanafunzi wengine waliofuata waliopita hapo, nao walishika nyadhifa za juu katika serikali ya kikoloni ya Uingereza, hata baada ya uhuru.

Inafafanuliwa, Padri Alington aliamua kuchagua eneo la Magila ambalo lilikwishajulikana kutokana na alama ya msalaba uliowekwa na Dk Krapf.

Nyerere alianza masomo katika Shule ya Msingi Mwisenge, Musoma mwaka 1934 na baadaye akaendelea katika Shule ya Sekondari Tabora, iliyokuwa chini ya Wamisionari wakati huo.



Mzee Omari Kijazi, alishuhudia mkasa wakati huo akiwa mwanafunzi. **PICHA ZOTE: CHEJI BAKARI.**

**AKUTANA NA MWALIMU WAKE**

Mzee Omari Kijazi, leo hii ana umri wa miaka 69, ana simulizi ya kushuhduia ya Mwalimu Nyerere, yeye wakati huo akiwa mwanafunzi, zama hizo kukiwapo wanafunzi wenye umri mkubwa kwa kuchelewa kuanza shule, alikuwa na miaka 17.

Anasimulia Nyerere, akiwa na miaka 11 ya kuongoza nchi, alifika eneo la kwao kufungua Mgodi wa Kufua Umeme wa Hale na kwa utamaduni wakati huo, walimu walikuwa na nafasi yao kukusanyika kuandaa mapokezi hayo ya kiheshima.

"Sisi wanafunzi (wa Shule ya Msingi Songa - Muheza) tulikuwa tumejipanga kwenye mistari, huku tukipiga makofi wakati anapita. Mara akatokea mzee mmoja anaitwa Galo, alikuwa na matatizo ya akili, mara naye akaingia kumkubatia Nyerere

"Watu wa usalama wakamfuata na kumtoa, Mwalimu Nyerere aliwakataza akasema 'muachieni, huyo ndiye Mwalimu wangu aliyenifundisha na amesomea kule Magila Msalabani Muheza!' Ndipo wote tulipatwa na butwaa," anasimulia Mzee Kijazi, akifafanua ni tukio ambalo likazidi kuiongezea hadhi shule hiyo kongwe nchini.

Nipashe
Spotika



USIYOYAJUA WAPINZANI WA SIMBA, YANGA CAF UK. 14



MASSIMILIANO-ALLEGRI

# MAKOCHA WANAOWEZA KUMRITHI ERIC TEN HAG

**MANCHESTER, England**

BAADA ya kustahimili mwanzo mbaya zaidi kuwahi kutokea kwa msimu wa Ligi Kuu England, inaonekana maandishi yanaweza kuwa ukutani kwa Erik ten Hag huko Manchester United.

Kocha huyo wa Uholanzi ameshinda mataji mawili katika klabu hiyo, hata hivyo hali ya ligi kwa Mashetani Wekundu imekuwa ya wasiwasi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na hajaonyesha dalili zozote za kuimarika licha ya kiasi kikubwa cha fedha kilichotolewa kusajili wachezaji wapya.

Huku Ten Hag akionekana kuishiwa na wakati United, 90min imechungulia orodha ya makocha wasio na ajira kwa sasa ili kuona ni nani klabu inaweza kumnasa.

**MASSIMILIANO ALLEGRI**

Manchester United kwa sasa wana matatizo mawili makubwa, hawafungi magoli ya kutosha na wanaruhusu magoli mengi sana.

Ingawa Massimiliano Allegri angefaa sana kurekebisha tatizo la kwanza, bila shaka angerekebisha la pili. Kocha huyo wa Italia ni mtaalamu wa mikakati mahiri katika safu ya ulinzi, na kuifanya Juventus kuwa karibu kutoweza kupenyeka katika vipindi vyake viwili katika klabu (hasa cha kwanza).

Takwimu zinathibitisha hivyo. Timu zake zimeshika nafasi ya pili katika historia ya Serie A, na alifurahia vipindi viwili ambavyo Juve hawakuruhusu bao hata moja kwa mechi 10 mfululizo. Ikilinganishwa na Man United walicheza mechi tisa pekee katika msimu mzima wa Ligi Kuu England 2023/24 chini ya Erik ten Hag.

Na ingawa soka lake linaweza lisiwe zuri, medali 10 za washindi wa Serie A na Coppa Italia alizonazo katika kabati lake la makombe ni dhibitisho kocha mzuri.

**GARETH SOUTHGATE**

Kipenzi cha Dan Ashworth, Gareth Southgate alihusishwa na uwezekano wa kuhamia Manchester United kwenye uongozi wa klabu mwishoni mwa msimu uliopita.

Na ingawa mashabiki wengi wa United wa England labda hawangefurahishwa sana na uteuzi huo - kutokana na kiasi cha mbinu za Southgate alizopokea katika ngazi ya kimataifa - upangaji wa mashambulizi ya kaunta wa kocha huyo huenda ungefanya kazi Old Trafford.

Kama tulivyoona hapo awali, mastaa kama Marcus Rashford na Bruno Fernandes wanafanya vyema katika mfumo wa mashambulizi ya kaunta, ambao ungefaidika zaidi na wachezaji bora wa United - jambo ambalo Ten Hag ameshindwa kufanya kwa muda wa miezi 18 iliyopita.

**THOMAS TUCHEL**

Kocha mwingine ambaye amekuwa akihusishwa na kuinoa United ni Thomas Tuchel bila shaka atakuwa uteuzi wa hali ya juu.

Mjerumani huyo ameongoza baadhi ya klabu za juu zaidi duniani, Bayern Munich, Chelsea, Paris Saint-Germain na Borussia Dortmund, na ameshinda makombe katika kila moja kati ya hizo.

Anaweza kuwa mjanja, lakini labda hivyo ndivyo kikosi cha United kinahitaji kocha ambaye atachukua mbinu isiyo ya kipuuzi.

**RUUD Van NISTERLROOY**

Uteuzi rahisi zaidi, Ruud van Nistelrooy tayari yuko kwenye klabu na kwa sasa anafanya kazi kama Kocha Msaidizi hapo Old Trafford.

Akiwa ameshinda Kombe la KNVB kama Kocha Mkuu alipokuwa na PSV Eindhoven miaka michache iliyopita, Van Nistelrooy ameonyesha ahadi kama kocha wa siku zijazo.

Anaweza kuwa uteuzi mwingine wa kuacha pengo la Ole Gunnar Solskjaer katika klabu hiyo ambayo, kutokana na jinsi raia huyo wa Norway alivyofanya vizuri katika miezi michache ya kwanza ya umiliki, inaweza kuwa si jambo baya.

## ISIKUPITE

WAMILIKI wa Klabu Al-Nassr ya Saudi Arabia wanaamini watafanikiwa kumsajili kiungo wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin de Bruyne, mwenye umri wa miaka 33, mara mkataba wake wa sasa utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu, kutokana na dau kubwa ambalo wamemwandalia.



## Extra Time



RONALDO



BECKHAM

VICTORIA BECKHAM

# WANASOKA 11 AMBAO WANA USHAWISHI KWENYE MITINDO

**LONDON, England**

WANASOKA wa kisasa hawaogopi kujieleza linapokuja suala la mitindo.

Sio tena waigizaji na wasanii pekee wanaopamba tamasha kwenye hafla mbalimbali za mitindo, wachezaji wa mpira wa miguu tuwapendao wanakumbatia fursa za kuingia katika ulimwengu wa mitindo, wakivalia bidhaa za kifahari huku wakionyesha upande mwingine tofauti na wanapokuwa uwanjani.

Kuanzia wachezaji kama hayati Pele na David Beckham, hadi nyota wa sasa Bukayo Saka na Marcus Rashford, wanasoka wanazidi kuwa na ushawishi mkubwa kwenye jukwaa la mitindo.

Hawa ndio wanasoka 11 wenye ushawishi mkubwa kwenye mitindo kwa mujibu wa 90min.

### 11. MOHAMED SALAH

Mohamed Salah ni mfalme wa soka ndani na nje ya uwanja. Yeye huvaa kila vizuri na ni mmoja wa wachezaji wanavaa vizuri zaidi kwenye mchezo.

Ubunifu wake umemruhusu kushiriki katika kampeni za mitindo za kusisimua, akipamba jarida la GQ katika mavazi ya kisasa na ya zamani.

### 10. MARCUS RASHFORD

Ikiwa ulitazama umati wa watu kwenye wiki ya mitindo ya Paris, unaweza kuwa ulimwona Rashford ameketi katika safu ya mbele ya onyesho la Louis Vuitton - nafasi ambayo amepata kwa haki.

Hakuna kitu ambacho Rashford hawezi kufanya. Yeye ni balozi kamili kwa kila mkusanyiko, kuleta mtindo, ukomavu na darasa nyingi kwenye jukwaa.

Kampeni yake ya kwanza ya mitindo ilikuja mwaka 2020, aliposhirikiana na Burberry kama balozi wao wa msimu wa baridi. Tangu wakati huo, ameendelea kusimama katika ulimwengu wa mitindo, akivunja vikwazo na maadili yenye changamoto.

### 9. TRENT ALEXANDER ARNOLD

Trent Alexander-Arnold, hebu sote tuchukue dakika moja kumheshimu.

Gwiji huyo wa Liverpool amekumbana na tasnia ya mitindo katika miaka ya hivi majuzi, pamoja kung'aa kwenye wiki ya mitindo ya Milan au kuvaa kabla ya kampeni mpya ya jeans ya Guess.

Chapa za Prada, Dolce na Gabbana na Burberry huwa zinamtumia kuonyesha uzinduzi wao mpya mara nyingi nyota huyu raia wa Uingereza.

Hajawahi kuogopa kushiriki mawazo yake pia, akimwambia Hypebeast: "Kuanzia kizazi changu kwenda chini, mitetemo sasa imetulia zaidi, haina mitindo wa zamani - na mradi tu wanacheza uwanjani, vijana wanaweza kufanya kile wanachotaka.

Ikiwa unatafuta nyota wa kisasa ambaye anafungua njia katika mtindo wa soka - hauhitaji kuangalia mbali zaidi ya Bukayo Saka.

Arsenal wanamjua katika ulimwengu wa mitindo, lakini Saka anaonekana kuwa mmoja wa wachezaji wabunifu zaidi wa kikosi hicho. Yeye daima ni mmoja wa wanamichezo wa kwanza kuonekana katika wiki mbalimbali za mitindo na ameiga baadhi ya mikusanyo ya kuvutia zaidi - ikiwa ni pamoja na Kampeni ya Burberry SS24.

Haishangazi anaendelea kuangazia mbele ya magazeti na matangazo ya mavazi ya kichwa.

### 7. SON HEUNG-MIN

Mchezaji wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min ni sawa na mwanamitindo wa soka, akionyesha darasa lake ndani na nje ya uwanja.

Mchezaji mpira mwingine anayependwa, Son akitumika katika chapa Burberry, Calvin Klein na TUMI. Mwonekano wake ni wa kudumu, uliowekwa pamoja na umaridadi - unamfanya kuwa mmoja wa wachezaji wa mbele zaidi wa mitindo kwenye mchezo.

### 6. CRISTIANO RONALDO

Ikiwa jina la Cristiano Ronaldo litaambatishwa kwenye chapa, bidhaa hiyo itauzwa kote ulimwenguni, haijalishi ni nini.

Jina lake ni chapa halisi, na kwa hivyo kujihusisha kwake na mitindo kunaleta maana kamili. Suti za hali ya juu, nguo za mitaani za kawaida na inafaa kwa michezo - Ronaldo anageuza vichwa na uhodari wake na vipande vilivyofikiriwa vizuri.

Hali yake kama 'aikoni' ya kweli imemwona akiunda tabia ya watumiaji na kushirikiana na kampuni nyingi. Kila mtu anataka kuwa Ronaldo.

### 5. DOMONIC CALVERT LEWIN

Jasiri shupavu - Dominic Calvert Lewin anawakilisha mtindo wa kufikiria mbele.

Calvert-Lewin amefungua mlango kwa maelfu ya wapiga mipira kujieleza, akipinga uamuzi na kukataa kunyamazishwa na miundo yake ya ajabu na mchanganyiko wa rangi.

Anastahili sifa kubwa kwa kazi yake katika ulimwengu wa mitindo. Yeye huwaangusha kila mara unyanyapaa kwa wapiga mpira wenzake, na kuwalazimisha watu kufikiria upya masimulizi yao kuhusu mitindo ya soka.

### 4. HECTOR BELLERIN

Wakati nyota wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Hector Bellerin, anaingia kwenye chumba, kila mtu anageuza kichwa chake. Hiyo sio tu kwa sababu ya kipaji chake uwanjani, lakini pia chaguzi zake nzuri za mavazi.

Bila shaka yeye ni mmoja wa wanaume maridadi zaidi katika soka, lakini ushawishi wake unapita zaidi ya mavazi anayochagua asubuhi. Beki huyo alizindua chapa yake mwenyewe ya mavazi endelevu mnamo Juni, akichonga nafasi mpya katika ulimwengu wa kandanda ambayo ina changamoto katika ubunifu.

### 3. JULES KOUNDE

Nyota wa Barcelona, Jules Kounde, hahitaji kabisa kutambulishwa. Ukijua mchezo wa mtu huyu, utajua ushawishi wake kwenye tasnia ya fasheni.

Hufika kwenye kambi za Barca kwa furaha kamili, wakitoka nje kwenye hafla za mavazi ya kusukuma mipaka na kushiriki katika kampeni za kisasa - Kounde haogopi kuwa mchafu, na ananufaika sana kutokana na ushujaa wake.

Hakuna kitu kisichowezekana kwa mlinzi huyo wa Ufaransa, na hivi karibuni angeweza hata kupanda safu ya orodha hii na umakini wake unaoendelea kwa ulimwengu wa mitindo.

Anacheza mstari kati ya mwanasoka na mwanamitindo, akikataa kujizuia wakati akifanya hivyo.

### 2. DAVID BECKHAM

Tunaweza kuacha sehemu hii ya makala yetu wazi, ushawishi wa Beckham kwenye ulimwengu wa mitindo sio hadithi mpya, bado anaendelea kufikia urefu mpya na kuvutia na mtazamo wake wa kufikiria mbele.

Siku zote alikuwa gwiji uwanjani - akijaribu mitindo ya nywele na mitindo ambayo ilikuwa kabla ya wakati wake. Sasa, uwezo wake wa kushawishi utumiaji unamfanya kuwa mali ya thamani sana kwa chapa nyingi.

Ikiwa David na Victoria Beckham watatikisa kwenye hafla ya mitindo, kamera zote zitawalenga wanandoa hao maarufu. Jina la Beckham halitawahi kutajwa katika mazungumzo sawa na mtindo wa soka.

### 1. PELE

Kulikuwa na mtu mmoja tu aliye juu ya orodha hii. Gwiji nje ya uwanja na juu yake, Pele alikuwa baba wa mitindo ya kandanda - akitengeneza mavazi ya kustaajabisha ambayo yalileta mtindo na kiwango.

Kazi yake ilikuwa inang'aa, lakini ushawishi wake nje ya uwanja ni ngumu kuweka kwa maneno. Mtindo wake ulikuwa wa kipekee - wa kipekee kwa njia ile ile ya uchezaji wake siku zote.

Sahau chapa za kifahari na mifumo inayotiliwa shaka - Pele alijua ni nini kilifanya kazi na kuifanya ionekane nzuri - akiibua kizazi cha wachezaji waliothubutu kutumbuiza katika ulimwengu wa mitindo.

## Nukuu

"Kadi nyekundu ni mbaya, haikupaswa kutokea. Lakini nina hasira sana kuhusu kadi nyekundu ya kwanza, wanasema nahodha ndiye pekee anayeweza kuzungumza na mwamuzi. Nikatembea hadi kwake, lakini sio kwa njia mbaya, hata kidogo na nikaambulia kadi." **alisema Virgil Van Dijk, nahodha wa Uholanzi.**



"Mmoja wa wachezaji wenzangu wenye uchawi mwingi na niliyefurahia kucheza naye pamoja Andres Iniesta, mpira utakukosa na sisi sote. Nakutakia kila la kheri." **Nahodha wa Argentina, Lionel Messi alisema baada ya nyota huyo mwenzake wa zamani wa Barcelona kutangaza kustaafu soka la kulipwa.**



"Hii imekuwa ikinisumbua sana katika maisha yangu kila kitu nilichofanya kazi kwa bidii kukipata kimesimamishwa. Nawashukuru wote kwa upendo na ushirikiano wenu kwa mara nyingine, Nasubiri kwa hamu kurejea tena uwanjani, " **kiungo wa Juventus, Paul Pogba, alisema.**





Kikosi cha MC Alger ya Algeria ambacho kinatarajia kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika. MC Alger iko Kundi A pamoja na wawakilishi wa Tanzania Bara, Yanga. **PICHA: MTANDAO**

# USIYOYAJUA WAPINZANI WA SIMBA, YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanyika kwa droo ya hatua ya makundi, tayari wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika wameanza maandalizi.

Yanga imepangwa Kundi A katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Al Hilal (Sudan) na MC Alger ya Algeria huku Simba ambayo itacheza mashindano ya Kombe la Shirikisho iko Kundi B na Bravo do Maquis ya Angola, CS Coastantine ya Algeria na CS Sfaxien ya Tunisia.

Si wengi wanaojua njia gani zimepita timu hizo hadi kutinga hatua hiyo, lakini pia rekodi zao katika michuano wanayocheza.

Pia hakuna anayejua vyema maendeleo yao kwenye Ligi Kuu za nchi zao katika msimu huu unaondelea.

Mwandishi wa makala haya, anakuletea kila kitu ambacho kitakufanya uzijue timu hizi zimefikaje hatua ya makundi, rekodi zao kwenye michuano na msimu huu zifanya nini kwenye ligi za nchini zao.

**TP MAZEMBE**

Ndiyo timu yenye rekodi nzuri zaidi katika Kundi A, ambalo lina wawakilishi wa Tanzania, Yanga.

Imetwaa taji hilo la Ligi ya Mabingwa mara tano, ikifanya hivyo 1967, 1968, wakati huo likiitwa Kombe la Klabu Bingwa Afrika, 2009, 2010 na 2015.

Imefika hatua ya fainali mara mbili, 1969 na 1970, imecheza nusu fainali ya ligi hiyo mara nne (2002, 2012, 2014 na 2018/19), huku ikifanikiwa kucheza hatua ya robo fainali mara mbili, 2018/2019 na 2019/2020.

Timu hiyo imetinga hatua ya makundi ilicheza mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Red Arrows ya Zambia, ikishinda mabao 2-0 ugenini, na kushinda tena nyumbani mabao 2-1, hivyo kutinga makundi kwa jumla ya magoli 4-1.

Haikuwa kwenye kiwango kizuri misimu miwili iliyopita, lakini imeboresha kikosi chake msimu huu kwa kufanya usajili bora na kurejea kule ilikokuzoea.

Mpaka sasa imecheza mchezo mmoja tu kwenye ligi ya nchini kwao, Oktoba 5, mwaka huu dhidi ya Malole na kulazimishwa sare ya bao 1-1 ikiwa nyumbani.

**AL HILAL**

Jina lake kamili inaitwa, Al Hilal Omdurman yenye maskani yake nchini Sudan. Ni moja kati ya timu zenye rekodi nzuri ya kucheza mara nyingi hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Imecheza Ligi ya Mabingwa Afrika mara 39, tangu ikiitwa Klabu Bingwa Afrika, lakini mara zote haijawahi kutwaa taji hilo.

Hata hivyo, ina rekodi ya kufika fainali mara mbili (1987 na 1992), pia ikitoa mfungaji bora Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2011, wakati straika wa timu hiyo, Edward Sadomba, raia wa Zimbabwe, alipopachika mabao saba na kutwaa kiatu cha dhahabu.

Imetinga nusu fainali mara nne, robo fainali mara mbili, ikiishia hatua ya makundi mara tisa.

Msimu huu imeweka rekodi ya kutinga hatua ya makundi mara sita mfululizo, mara baada ya kuichapa Al Ahly Benghazi ya Libya ikicheza ugenini na sare ya bao 1-1 ikicheza Sudan Kusini.

Kwa misimu miwili sasa haichezi ligi nyumbani kwao kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe, badala yake inacheza ligi nchini Mauritania na imeshinda michezo yote miwili iliyokipiga nchini humo, ikiichapa Inter Noakchot mabao mabao 4-1, na magoli 5-0 ikiwaadhibu Nzidane.

**MC ALGER**

Inaitwa Mouloudia Club d'Alger, kifupi MC Alger ya Algeria. Imeshawahi kutwaa ubingwa huo, lakini ikiwa ni mwaka 1976, ikifika hatua ya robo fainali mara tatu, 1977, 1980 na 202, ikishiriki michuano hiyo mara tisa.

Imeanza michuano hiyo raundi za awali kama Yanga, ikiiondoka Watanga FC ya Libya kwa jumla ya mabao 4-0, ikishinda mabao 2-0 nyumbani na na ushindi kama huo ugenini.

Timu hiyo inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Algeria, ikicheza michezo minne, ikishinda miwili na sare mbili, ikiwa na pointi nane, nyuma ya Olympique Akbou, inayoongoza kwa pointi tisa.

**BRAVOS DO MAQIS**

Hawa ni wawakilishi wa Angola katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, wakiwa kundi moja ya Simba.

Haina rekodi yoyote ya kuvutia kwenye soka la nchi hiyo, lakini imefanikiwa kucheza michuano hiyo kwa kutwaa Kombe la FA nchini humo msimu uliomalizika.

Njia iliyopitia ni kuiondoka Coastal Union ya Tanzania kwa kuifunga mabao 3-0, iliyotapata ikicheza nyumbani, kabla ya kulazimishwa suluhu waliporudiana hapa nchini kwenye hatua ya raundi za awali.

Raundi ya kwanza ilicheza na FC Lupopo ya DR Congo, ikishinda bao 1-0 nyumbani, kabla ya kwenda kushinda tena ugenini kwa magoli 2-1.

Kwenye ligi nchini mwake inakamata nafasi ya tisa, ikicheza mechi nne, kushinda moma, sare mbili, ikipoteza moja, mchezo wa mwisho ikipigwa mabao 2-0 dhidi ya Petro de Luanda.

**CS COSTATINE**

Ni moja ya timu ambazo kwa sasa zinasumbua kwenye ligi ya Algeria, ingawa haina rekodi nzuri sana katika mashindano ya kimataifa.

Imecheza Kombe la Shirikisho mara mbili na zote ikiishia raundi ya pili, hivyo hii ni mara ya kwanza kutinga hatua ya makundi, ikiwa pamoja na Simba.

Ilianza mechi za awali kwa kuichapa, Polisi ya Rwanda mabao 2-0, na ikashinda tena ugenini mabao 2-1, hivyo kutinga raundi ya kwanza, ikakutana na Nsoatreman ya Ghana na kuinyuka mabao 2-0 ikicheza ugenini, ikashinda tena bao 1-0 ugenini na kutinga makundi. Inakamata nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini mwao ikiwa na pointi sita kwa michezo minne iliyocheza.

**CS SFAXIEN**

Imepangwa Kundi A katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, CS Sfaxien ndiyo timu yenye rekodi nzuri zaidi kuliko zote.

Imetwaa kombe hilo mara nne, mara moja wakati likiitwa Kombe la Washindi Afrika.

Ilianza kulitwaa 1998, baadaye ikafanya hivyo 2007, 2008, na 2013, wakati limeshabadilishwa jina la kuitwa Kombe la Shirikisho. Ilianza moja kwa moja kucheza raundi ya kwanza kama Simba, ikiichapa Rukinzo ya Burundi bao 1-0 ikiwa ugenini, na kushinda tena nyumbani bao 1-0, kabla ya kutinga makundi.

Kwenye Ligi Kuu nchini Tunisia ipo nafasi ya sita, ikicheza mechi nne, ikiwa na pointi saba mpaka sasa.

**JE, WAJUA?**



Enzo Maresca amekuwa kocha wa kwanza wa Chelsea tangu mwaka 2021, kutwaa tuzo ya Kocha Bora wa mwezi wa Ligi Kuu England. Maresca ametwaa tuzo ya Septemba baada ya kuifunga Bournemouth, West Ham na Brighton, huku akitoa sare ya bao 1-1 na Crystal Palace.

HABARI KITAIFA

## HaloPesa yatoa msaada kwa watoto wenye changamoto kichwa kikubwa

**Na Zuwena Shame**

KATIKA kusherehekea miaka minane tangu kuanzishwa kwake nchini, HaloPesa Tanzania imetoa misaada mbalimbali ya vyakula na mahitaji kwa watoto na wazazi katika taasisi ya Nyumba ya Matumaini ilichoko Kimara, mkoani Dar es Salaam.

Misaada imetolewa kwa wazazi/walezi na vijana wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Akizungumza kituoni huko jana, Kaimu Mkurugenzi wa HaloPesa, Magesa Wandwi alisema kuwa katika kuwajali wateja wao hasa watoto wenye uhitaji maalum, HaloPesa imeamua kuwapa faraja watoto na wazazi wa kituo kama njia moja ya kuonesha na kurudisha shukrani kwa jamii ya kitanzania.

Wandwi alisema Halopesa imeona uhitaji wa mahitaji ya wazazi na watoto hao kituoni huko, huku wakiwa wanasubiri matibabu.

"Kama HaloPesa, kuja kituoni hapa ni fursa kubwa kwetu. Na kama jamii tunahakikisha kuwa tunatumia mchango wetu kuendeleza ustawi wa watoto katika mazingira yao ya maisha ya kila siku," alisema Wandwi.

Alisema Halopesa inaamini kuwa watoto wenye uhitaji maalum ni kizazi na urithi wa Watanzania, hivyo kila taasisi ina jukumu la kuchangia watoto hao katika jamii.

Aliongeza kuwa kwa kutembelea kituo hicho, wafanyakazi wa HaloPesa wameona ni namna gani kila mmoja ana wajibu wa kushirikiana na wazazi na walezi wanaopitia changamoto mbalimbali kwa kupata wasaa wa kula chakula cha mchana na wazazi na watoto.

Mmoja ya wazazi wenye watoto wenye kichwa kikubwa kituoni huko, Fatuma Ali, aliishukuru Halopesa kwa kujua na kutatua changamoto wanazokabiliana nazo katika kulea watoto hao, akiwaomba wadau wengine kuiga mfano huo.

# NEMC yaonya kufunika chakula kwa kutumia mifuko ya plastiki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa onyo kwa mama ntilie kutumia mifuko ya plastiki kufunikia au kuhifadhia chakula, kwa kuwa ni hatari kwa afya na ni kosa kisheria.

Mwaka 2019 serikali ilipiga marufuku ya matumizi ya mifuko hiyo na ni kosa la jinai kutengeneza, kuuza, kusambaza na kutumia kwa mujibu wa kifungu cha 230(2)(f) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na Nipashe hivi karibuni, ulibaini mama ntilie hao wamekuwa wakipata mifuko hiyo, kwa wauzaji sukari (mfuko wa ndani ya mfuko wa sukari), kwa ajili ya kufunikia chakula.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa NEMC, Irene John, alitoa onyo hilo jana jijini hapa, wakati wa mafunzo ya masuala ya mazingira kwa kikundi cha Wanawake na Samia mkoani Dodoma.

Alisema serikali ilishachukua hatua za kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kutokana na athari za kiafya, ikiwamo kuchangia watu kupata saratani.

"Ninyi Wanawake na Samia, nendeni mkawe mabalozi mtoe elimu kwa wananchi hasa mama ntilie wajiepushe na matumizi ya mifuko hiyo, lakini pia kutokana na katazo la serikali matumizi ya mifuko ya plastiki, tumieni fursa kwenu kutengeneza mifuko mbadala, ili kujikwamua kiuchumi na kutunza mazingira," alisema.

Akitoa mada mbalimbali kwenye mafunzo hayo, Ofisa Mazingira Mkuu wa NEMC Kanda ya Kati, Ahmad Mbwana, alisema mifuko ya plastiki inapopata joto hulainika na kusababisha chembechembe za kemikali kuingia katika chakula na kuhatarisha afya ya mlaji.

"Mifuko hii ina kemikali ambazo zikiingia katika mwili wa binadamu zinasadikika kuleta saratani na baadhi ya viungo kushindwa kufanya kazi ipasavyo," alisema.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Dk. Careen Kahangwa, alisema wanawake hao wamepatiwa mafunzo mbalimbali ikiwamo sheria na sera za mazingira, ili kuwa mabalozi wa utunzaji mazingira katika maeneo yao.

"Tunawaelimisha wanawake kwa kuwa ukimwelimisha mwanamke umeelimisha jamii, tunaamini ninyi ni rahisi kusukuma ajenda ya mazingira, tunataka kwa sasa mhakikishe mnaongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kuunga mkono maono ya Rais Samia kwenye kulinda mazingira yetu," alisema.

Mwenyekiti wa Wanawake na Samia mkoani humo, Fatuma Madidi alishukuru NEMC, kwa kutoa elimu hiyo na kwamba fursa za mazingira watazitumia ipasavyo kwa kuhamasisha wanawake wengine kwenye maeneo yao kujikwamua kiuchumi.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bw. Adolf Nduguru (wa pili kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mwongozo wa uanzishwaji na usimamizi wa kampuni mahsusi za uendeshaji wa miradi ya vitega uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika hafla iliyofanyika mjini Dodoma, jana. Wanaoshuhudia kutoka kushoto ni, Johnson Nyella, Kamishna wa Sera wa Wizara ya Fedha, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa wizara hiyo; Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji nchini (UNCDF), Peter Malika na kulia ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa TAMISEMI, John Cheyo.

# Wasiojulikana wabomoa madarasa ya shule mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAHARUKI imetanda miongoni mwa wakazi wa kata ya Tembela, jijini Mbeya, baada ya watu wasiojulikana kubomoa madarasa ya shule mpya inayojengwa kwa nguvu za wananchi katika kata hiyo.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki, wananchi wakidai majengo hayo yalibomolewa usiku wakiwa wamelala, hivyo kurudisha nyuma juhudi zao na za serikali kuboresha sekta ya elimu.

Mmoja wa wananchi hao, Tamson Kasanga, alisema shule hiyo inajengwa na wananchi kwa kuchangishana fedha na kwamba katika eneo hilo hakuna mgogoro wowote wa ardhi na hivyo hawajui sababu za watu hao kubomoa madarasa.

Alisema wao ni wakulima na hivyo huwa wanachangishana kila mwananchi Sh. 12,000 ambazo kwa sehemu kubwa zinatokana na biashara ya mazao wanayolima.

"Kitendo hiki kimetushtusha sana, sisi hatuna vyanzo vikubwa vya mapato zaidi ya kilimo ambacho ni cha msimu, tumeshindwa kuelewa hawa watu wana nia gani kwa sababu hapa hapana mgogoro wowote wa ardhi, kwamba useme ndio unaosababisha," alidai Kasanga.

Mashaka Mwashembela, ambaye ni mzee wa mila wa eneo hilo, alisema kuwa baada ya kutokea tukio hilo viongozi wa serikali walishirikishwa na kuanza kufuatilia lakini hawajawabaini wahalifu hao.

Alisema jambo hilo halijawahi kutokea katika eneo hilo na hivyo limewashtua wananchi pamoja na viongozi wa serikali na akawatahadharisha wahalifu hao kwamba wanapaswa kuacha mara moja kwa kuwa "watawashughulikia".

Diwani wa Tembela, Frank Mwasyoke alisema ujenzi wa madarasa ya shule hiyo umegawanywa kwa kila mtaa kupatiwa jengo moja wakati wanasubiri nguvu ya serikali.

Alisema awali lilianza kubomolewa jengo la mtaa wa Tembela na baadaye likabomolewa jengo la mtaa wa Relini na kwamba majengo hayo yalibomolewa kwa siku tofauti.

Alisema kuwa awali baada ya jengo la mtaa wa Tembela kubomolewa walidhani lilikuwa limejengwa chini ya kiwango na hivyo likabomolewa na upepo lakini wakabaini kwamba ni watu wanafanya hivyo baada ya jengo la mtaa wa Relini kubomolewa.

"Jengo hili la mtaa wa relini lilikuwa lipo chini kiasi kwamba hata mnyama akiegemea asingeweza kubomoa na hapa ndipo tulipogundua kwamba ni watu wanabomoa, sasa hatujui nia yao ni nini lakini hali hii inakatisha tamaa wananchi," alisema Mwasyoke.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Annamary Joseph, alisema kuwa baada ya kupata taarifa za tukio hilo, alikwenda na wataalamu wa jiji hilo, kutembelea eneo hilo na kufanya vikao na viongozi wa kata hiyo pamoja na viongozi wa shule.

Alisema waliamua kuanza kuchukua hatua za awali za kudhibiti uhalifu huo, kwa kuagiza aajiriwe mlinzi ambaye atakuwa anaangalia usalama wa eneo hilo.

Alisema juhudi za kumpata mlinzi huyo zinaendelea kufanywa na viongozi wa shule, kwa kushirikiana na wa kata huku akiwataka wahalifu hao kuacha tabia hiyo kwa kuwa haina tija katika jamii zaidi ya kurudisha nyuma maendeleo.

# Jaji Warioba: Alilenga mambo matatu, alichosema alimaanisha, je viongozi leo?

**Na Christina Mwakangale**

INAPOTIMIA miaka 25 bila uwapo wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, anakumbukwa kwa misingi aliyoiweka ambayo bado inaenziwa.

Kati ya viongozi ambao walikuwa katika Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere, hukosi kumtaja Jaji Joseph Warioba, akishika nyadhifa tofauti wakati huo.

Kwa sasa, Jaji Warioba ni Waziri Mkuu mstafau wa Serikali ya Awamu ya Pili. Hivi karibuni Jaji Warioba, amezungumza na waandishi wa habari akieleza masuala kadhaa, ikiwamo kumgusa Mwalimu Nyerere, miaka 25 tangu kufariki kwake mwaka 1999 huko London, Uingereza.

Jaji Warioba anasema Mwalimu Nyerere alikuwa na dira katika uongozi wake, kabla ya uhuru kwanza, ya kwanza ikiwapo inayolenga kuhakikisha uwapo wa utaifa. Anasema dira ya pili, baada ya uhuru ililenga maendeleo, kwa maana ya kuwaondoa aliowaita 'maadui watatu'; Ujinga, Maradhi na Umaskini.

Kadhalika ya tatu, Mwalimu Nyerere alilenga kuzilinda tunu za taifa anazozitaja kuwa ni; maadili, uzalendo na kupinga rushwa.

"Tuliupata uhuru kwa amani iliyotokana na sisi wananchi wenyewe na si kwa mtutu wa bunduki. Tuliondoa udini, ukanda na ukabila," anatamka Warioba.

Anasema uongozi wa Mwalimu Nyerere, ulibeba mambo ya msingi yaliyolipewa kipaumbelea, akitaja mojawapo ni umoja.

"Kwa mfano tuna umoja ambao hauwezi kuukuta katika nchi nyingi sana. Umoja ule ulijengwa katika hali ngumu, haikuwa rahisi lakini ulijengwa wakati wote.

'Ni wakati huo ambao tuliondoa uchifu, ndio wakati huo tuliondoa ubaguzi wa kidini, ndio wakati huo tulijenga muungano na tukajenga umoja wa nchi.

"Umoja ulijengwa kwa msingi wa haki za binadamu wote ni sawa, na dini ikawa msingi wa amani. Tunapozungumzia umoja, amani lazima umkumbuke Mwalimu," anasema Jaji Warioba.

Anaeleza kwamba hata katika maendeleo, ipo sura ya Mwalimu Nyerere, kwamba wakati wa harakati za kupata uhuru kulikuwako dira ambazo ni za utaifa na maendeleo.

"Ili tuendelee tulisema tuna maadui watatu, ujinga, maradhi... yaani, ili muendelee lazima uangalie maendeleo ya watu, umtoe mwananchi katika ujinga, umpunguzie maradhi na kumuondoa katika umaskini.

"Tutamkumbuka Mwalimu wa tunu, wakati wake suala la lilikuwa muhimu uzalendo, ulinzi wa nchi ilikuwa ni jukumu la kila mmoja, uongozi ulikuwa jumuishi," anaeleza.



Jaji Joseph Warioba akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni mkoani Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



Hayati Mwalimu Julius Nyerere

> Mwalimu alichokuwa anasema, alikuwa anamaanisha. Je, tujiulize sasa Watanzania, viongozi, tunachosema ndio tunamaanisha?

"Kwa maendeleo ya nchi, asingeweza kufanya kila kitu, ila aliweka misingi fulani fulani unabadili mambo fulani, huwezi kusema kwamba matatizo yote yataisha, hata Marekani yapo mambo ambayo yana matatizo,'anasisitiza Mzee Warioba.

"Mwalimu alichokuwa anasema, alikuwa anamaanisha. Je, tujiulize sasa Watanzania, viongozi, tunachosema ndio tunamaanisha?" anatoa mtazamo kwa lugha ya kuhoji.

Warioba anasema kwamba, wakati nchi ikielekea uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu (uandikishaji ukianza), ipo haja ya kuwapata viongozi wanaotatua matatizo ya wananchi, akisema taswira ya kiongozi ni yule anayewajibika kwa watu wake.

"Kwa kuwa maandalizi ya kuwafanya wananchi wawachague wanaowataka ni duni, licha ya kwamba wapigakura wa kitongoji ndio wanaowafahamu wanaoishi eneo lao, vyama vinapeleka watu wao (wateuliwa), wakati wa mfumo wa chama kimoja, kulikuwa na utaratibu wa kujua, Je, hawa wanakubalika?

"Kulikuwa na mkutano mkuu kwa ajili ya kupata kura za maoni, lakini ikaja hoja mkutano mzima unaweza kuhongwa, tuite wote balozi hadi wenyeviti wa wilaya waje.

Lakini haikupita muda kumbe hata kundi hili kubwa kuna watu wana fedha nyingi wanaweza kuwahonga, tuite wanachama wote bado ikashindikana."

Tatizo la rushwa sasa, Jaji Warioba analitaja sasa ni kati ya alivyovikemea Mwalimu, lakini baadhi ya maeneo likawa linaingilia uchaguzi.

"Tukasema tuwe na wajumbe wa kupiga kura za maoni, bado tatizo," anasema Jaji Warioba na kuendelea: "Kwa hiyo hatuna uhakika tuliposema wananchi wana haki ya kumpata yule wanayemuona anafaa.

"Katika maandalizi, vyama vya siasa viwe na utaratibu ambao unazingatia wanaoteuliwa wanakubalika kwenye maeneo yao, kwa sababu wakichaguliwa wasiofaa hawatasaidia.

"Kwa sababu akiwa mteuliwa na chama, lakini hakubaliki inawapunguzia uwezo hawa viongozi, wananchi hawamkubali, inakuwa ngumu kuwaongoza, tunataka watu wanaokubalika na jamii."

Jaji Warioba, anfafanua kwamba, uongozi kwenye serikali za mitaa ni muhimu, akikumbuka zamani balozi wa kitongoji alivyokuwa na nguvu, kutokana na kwamba ndiko kunakoanzia uongozi.

**RAIS AWATATUTULIE SHIDA**

Anasema, katika ngazi ya chini kutokuwa thabiti imekuwa sababu ya jamii inapotokea tatizo, kuitazama nafasi ya juu kiuongozi wakimtaka rais awatatulie matatizo yao.

Pia, anashauri haja ya serikali na mamlaka za usimamizi wa uchaguzi kukaa meza moja na vyama vya siasa, kuvihakikishia amani, akionya matumizi ya nguvu ya vyombo vya ulinzi na usalama, tija yake hupungua kutokana na pande zote kushindana.

Jaji Warioba anasema, kwa kipindi cha takribani miongo mitatu demokrasia imejengwa, ingawa utawala bora uliwekwa nyuma na kwamba ni wakati wa kuujenga, kwa kuwa ndio msingi wa uongozi.

"Miaka mitatu iliyopita hali ya siasa haikuwa nzuri, maandamano yalizuiwa, mikutano...amejenga na rais ameweza nchi sasa imetulia, kwa sababu aliondoa yale matatizo. Mfano haya maandamano ya hivi karibuni mimi ninachokiona ni kupambana.

"Jeshi la Polisi linasema watakaokuja watakiona, vyama vya siasa nao wanakuja na wanachokitaka, watumie lugha nzuri katika shughuli za siasa zetu. Amani inajengwa na wananchi, sio polisi peke yao maana wanasema wanalinda amani, mi nadhani wakae chini pande zote, wakubaliane," alisema.

# Aliibua CSR kwa burudani na michezo, Awamu Sita imejikita miradi ya jamii

**Na Peter Orwa**

• Chimbuko muziki Bima, Sikinde; klabu soka Tumbaku...

KATIKA hotuba yake wakati Tanganyika inapata uhuru, Rais Julius Nyerere alisisitiza kwamba "watawala wa Kiingereza waliodai awali hatuwezi kujitawala, waje baada ya miaka 10 kuona mabadiliko yaliyofikiwa."

Ni hoja na dhana iliyoshuhudiwa kwa matendo baadaye miaka hiyo kuanzia 1970, nchi ikiwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mipango ya Maendeleo nchini baada ya miaka saba kutimu 1961, kulishuhudiwa hatua kubwa kwa sekta zote zikiwamo mapinduzi kwenye mihimili mikuu ya uchumi kama kilimo na kwenye kazi za uzalishaji viwandani.

Wakati huo, Tanzania inatekeleza Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo, 1969 - 1974, maboresho ya kilimo cha kisasa ilihuisha zaidi maisha asilimia 85 ya Watanzania waliokuwa wakulima, ndipo Rais Nyerere akachukua nadharia inayomea sasa ya CSR (Corporate Social Responsibility), akiwarejeshea Watanzania mavuno ya mbegu ya uhuru wao mwaka 1961.

CSR ikiwa na maana kitaalamu, taasisi kuwajibikia jamii kwa kuirejeshea sehemu ya inachokivuna, inatajwa moja ya manufaa yake ni kuiwezesha taasisi kuzoea mazingira, pia kuzoeana na wenyeji.

Katika mustakabali huo, inafungua ubia kati ya wawekezaji na wanufaika wakipata watumishi bora, wateja na kukubalika, huku kukisambazwa ujuzi na mfumo wa utawala kuwafikia wenyeji.

Katika mawanda mapana, CSR inaboresha mfumo wa serikali kwa umma, sheria na kanuni zake na kueneza uhusiano wao.



Jengo kongwe mojawapo la Shule ya Msingi Mwisenge, Musoma alikoanzia masomo Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1934. **PICHA ZOTE: MAKTABA**




Ubao wa ofisini wenye orodha ya wanafunzi maarufu walipitia shuleni Mwisenge, alikosoma Rais Julius Nyerere.

### ALICHOFANYA NYERERE

Kufika mwaka 1970 ukiwa mwaka mmoja baada ya kuundwa Sheria Maalum ya Mashirika ya Umma na Wafanyakazi, maarufu SCOPO, ubunifu wa Nyerere aliouwasilisha katika kikao kikuu cha TANU, kukapitishwa agizo la kuundwa mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi.

Ubunifu huo ulioasisiwa na Mwalimu Nyerere, ulikuwa na sura ya CSR, kuwarejeshea wafanyakazi wanachowajibikia.

Kama hilo, TANU ikapitisha Azimio la Iringa 1972 na ajenda 'Siasa ni Kilimo' iliyokuwa na jozi ya kuboresha kilimo, ndani yake ikiwamo 'Operesheni Vijiji vya Ujamaa' mwaka 1974.

Rais Nyerere katika mkakati wake Vijiji vya Ujamaa vilivyolenga kukusanya manufaa ya watu na kisha kuwa na uzalishaji wa pamoja kwa manufaa ya wote, pia ukawa ulingo wa serikali kuwekeza maendeleo ya pamoja mahali waliko, kama vile shule na zahanati.

Mwaka 1973, katika kumrejea mtu wa chini aliko, tafsiri ya Maendeleo ya Viwanda ikashushwa chini umma uliko, kwa kuundwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), kuhamasisha maendeleo ya viwanda vidogo vijijini na mijini.

Ndani ya mwaka huo, ndio kukashuhudiwa mapinduzi makubwa moja kwa moja, pale Rais Nyerere alipoelekeza kuwekwa huduma za kijamii hasa za burudani katika mifumo rasmi ya utendaji.

Hiyo ilitokana na hali tofauti na sasa, wakati huo baadhi ya huduma za jamii za lazima zilitolewa bure ikiwamo ya afya. Maelekezo hayo ya Nyerere, yakawa sababu kuanzia mwaka 1973, kukaonekana mathalan CSR za bendi za muziki wa dansi, ambayo ilikuwa burudani kuu iliyotawala nchini.

Hata zinapotajwa Bendi za Muziki wa Dansi za Urafiki wana - Chakachua iliyoanza mwanzoni mwa miaka ya 1970, kisha baadaye Biashara Jazz Band, ikaja bendi za DDC Mlimani Park na Bima Lee Orchestre, ni sehemu ya uwekezaji huo katika mashirika ya umma nchini, kuhitimisha CSR zikijumuika na wakongwe NUTA Jazz - Msondo, huku vilabu vya soka na mpira wa pete vikimea kila kona katika taasisi za umma.

Hapo kuna timu za soka kama Tumbaku (Morogoro), Pamba (Mwanza), Usalama (mjumuiko vikosi vya Usalama) na TCC- Sigara ya Dar es Salaam, ambayo pia zilikuwa na timu mahiri ya pete.

Mifano mingine ilikuwa timu za mpira wa pete, ni Bima (NIC) na Jeshi Stars (JWTZ), chombo cha umma kilichosheheni nguzo zote za michezo, kwa namna ya pekee iking'aaa katika riadha kuwaibua (sasa wastaafu) Meja Filbert Bay na Kanali Juma Ikangaa, waliolipaisha Taifa kimataifa wakitwaa medali kadhaa.

Vilevile muda mrefu zilishakuwa na bendi maarufu za muziki Mwenge Jazz 'wana- Paselepa' ya JWTZ, pia JKT Kimbunga Stereo ya Dar es Salaam na JKT Kimulimuli ya Mafinga, Iringa; huku Polisi nayo ikinesa na bendi yake ya 'wanavangavanga' na Uhamiaji 'wana -hamahama.'

Hapana shaka, Tanzania katika michezo na burudani ikawa maradufu, hata mpira wa vikapu timu kama Benki Kuu (BoT) ilikuwa tishio na nyota wake vijana wakati huo, kama Stephen Mbundi, ambaye sasa ni Katibu Mkuu wizarani na Bima (NIC) yenye mshambuliaji Adam Kasidi 'Hunter'. Bima pia ikawa imesheheni burudani zote, zikiwamo hata muziki wa taarabu na ngoma za asili, pia klabu soka .

Vilevile mpira wa pete NIC ilikuwa 'haijambo', kitaifa Tanzania ilikuwa tishio kutwaa ubingwa wa Afrika Mashariki ikiwa na nyota wake kama vile Amina, Chijumba na Judith Chifupa, kukimea majina yao kimichezo kama vile 'wifi'.

Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) wakati huo ikiwa shirika la umma, ilisheheni huduma kwa jamii yenye wajibu inayoonekana kuwekezwa kimasoko katika zama za Uchumi Huria, ikiwa chombo kilichobinafsishwa.

Kutokana na ukubwa huo wa michezo, kukaundwa Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma (SHIMMUTA) kila kukifika msimu wake ulitikisa nchi, vilabu vikubwa vya soka nchini vilifika hapo 'kukodoa macho' ya kuiba wachezaji mahiri.

Ni aina ya CSR ikaendelezwa pia na wajenzi wa reli ya TAZARA hasa wataalamu wa Kichina waliokuwa wamaonyesha sinema katika maeneo ya wazi, mfano ndani ya Dar es Salaam jirani na stesheni kuu, akikumbukwa mwonyesha sinema wakati huo, mara mbili kila wiki, Mchina Ro-Lee.

Tafsiri inayoegemea hapo ni utashi wa kunufaisha watu na taasisi yao ya umma, kukikumbukwa watu waliendа kuona katika kumbi mbalimbali kama vile Avalon na Empire, Dar es Salaam.

Ilifika hatua hata kampuni binafsi zikachukua mkondo huo, mathalan wauza dawa kutoka Kenya kama vile 'Cafenol' na waonyesha sinema iitwayo "Factual Film' walifanya hivyo kila mwezi Dar es Salaam, katika miaka ya 1970 katika viwanja vya wazi, mkabala na Kituo cha Polisi Chang'ombe.

Msingi wa CSR hiyo kutolewa na serikali, ina ufafanuzi wake kisiasa unaotolewa na mwanazuoni wa kigeni wa sayansi ya Dk. Alfred Lokuji (sasa profesa), wakati fulani akiwa nchini, alitumia matamshi:

"Katika mfumo wa kisiasa wa mrengo wa kushoto (Ujamaa), serikali inabaki kuwa sehemu ya jamii, daima haitawaacha waelemewe na nguvu za soko (ikiwamo katika burudani), serikali inawajibika kuwahudumia..."

### MAGEUZI CSR

Mageuzi makubwa ya kiuchumi yakashuhudiwa baada ya kustaafu Mwalimu Julius Nyerere katika uongozi wa Mzee Ali Hassan Mwinyi, Tanzania ikiingia rasmi kisera, kisheria na kiuchumi katika uchumi wa soko na siasa huria.

Mabadiliko hayo yaliyopitia awamu kadhaa za uongozi, hadi kufika Awamu ya Sita, sasa CSR ikazama ndani ya mfumo wa kuwawajibisha wawekezaji, kujikita katika kuwa na miradi ya kuiwajibikia jamii, ione inavyonufaika. Mathalan, hivi sasa Kituo cha Uwekezaji na sera rasmi ya kuwawajibisha kwa CSR, umma unufaike.

> Katika mfumo wa kisiasa wa mrengo wa kushoto (Ujamaa), serikali inabaki kuwa sehemu ya jamii, daima haitawaacha waelemewe na nguvu za soko (ikiwamo katika burudani), serikali inawajibika kuwahudumia...

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**KULTHUM SHAIBU KHAMISI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4592-0019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIPATA ISLAMIC SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/220404/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**Joseph Thomas Sinyaw** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE189017** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 10 Septemba 2019. Mwisho wa matumizi ni tarehe 09 Septemba 2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/26012/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AUGUSTINO RAPHAEL MKUCHI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S.1318-0052** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NANDEMBO SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/RUV/TUN/7306/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MABEL IDD MASASI**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T137 CNB** AINA YA PICK UP RANGI NYEUPE YENYE CHASISI NAMBA **KM510032752.**
KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE
POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/15710/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AZIZ SHABANI SWAI**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 744 DLN – TOYOTA COASTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**PHQ/DAR/UBU/219435/2024.**

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 19502 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JAMES MNGODO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MICHAEL JAMES MNGODO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of 10...2024
Dated at Dar es salaam this 15 day of 08...2024.

Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.41/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JANETH SUMILE MABWAHI wa NYUKA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JOYCE JOSHUA SUMILE**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe ... Mwezi ... Mwaka ...

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25402/2024**

**In the matter of the Estate of the late ELIAS JACOBO TEETE of Oysterbay Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DOUGLAS ELIAS TEETE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 Day of 11, 2024
Dated at Dodoma this 10 Day of 10, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**SHASHINHALE AUCTION MART AND COURT BROKERS LTD**
**(Dealers in court Broker, Debt Collectors and Commission agent)**
**TEL:0757006076, P.O.BOX 288 – GEITA**

**TANGAZO LA MNADA WA GARI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 14274/2024**

**THE BOARD OF TRUSTEES OF THE NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND (NSSF)..................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**KIRIBO LTD..................................................................MDAIWA**

**KWA AMRI TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI GEITA, TUTAUZA MALI YA MDAIWA KIRIBO LTD AMBAYO NI GARI MAKE MAN YENYE NAMBA ZA USAJIRI REG T.383 CCD**

**TAREHE YA MNADA : 18/10/2024**

**MUDA WA MNADA : SAA 3:00 ASUBUHI**

**SIKU YA MNADA: IJUMAA**

**ENEO LA MNADA: mwatuloye, yard 2**

**MASHARTI YA MNADA**
MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA 25% YA PESA ITAKAYOFANYIKA MARA TU NYUNDO YA MTEKELEZAJI ITAKAPOMUANGUKIA, NA 75% ILIPWE NDANI YA SIKU KUMI NANNE (14) TOKA SIKU YA MNADA TOIFAUTI NA HIVYO 25% HAITARUDISHWA ITAINGIA KWENYE GHARAMA ZA UTEKELEZAJI NA MNADA UTATANGAZWA UPYA. PIA UNARUHUSIWA KULIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA.

**WOTE MNAKARIBISHWA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya GEITA**

**Kituo cha KATORO Mkoa GEITA**

**Shuri la Madai/ Ndoa Na 81/2022**

**Jina la mdai ..........................KAPAYA S/O/ DOTTO**

**Jina la mdaiwa.................. (1) FITINA S/O JUMA**
**(2) SALOME S/O ZEFANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji masahuri mahkama za Mwanzo)**

**Kwa (1) FITINA S/O JUMA (2) SALOME S/O ZEFANIA**

Kwamba mdai amaeleta maombi mbele ya mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya sahuri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya mahakama hii tarehe 17 mwezi 10 mwaka 2024 kueleza kwanini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama leo tarehe 4th mwezi 10 mwaka 2024

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**

**SHAKIRA LISUMA, POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI TAREHE 16/10/2024**

**SHAURI LA JINAI RUFAA NA.15609/2024**

**FURAHINI BENY KANYIKA.........MWOMBAJI RUFAA**

**DHIDI YA**

**SHAKIRA LISUMA....................MJIBU RUFAA**

Shauri la Rufaa ya Jinai tajwa hapo juu,limetokana na Shauri la Jinai Na.223/2024 Mahakama ya Mwanzo Boma. SHAKIRA LISUMA (Mjibu Rufaa) Popote ulipo unaarifiwa kuwa shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 16/10/2024 mbele ya Mh.R.Kasele-(PRM).

Unatakiwa kufika wewe wenyewe au muwakilishi wako bila kukosa na kwamba unatahadhalishwa kuwa endapo hautohudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa Uamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 09 Mwezi wa oktoba 2024.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MOROGORO

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25461 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the late JEREMIAH MGABISA MNYAWAMI of NKHUNGU within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BONIFACE JEREMIAH MNYAWAMI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 ............day of 11..................2024
Dated at Dodoma this 19th Day of July..............2024

.....................................
**PETITIONER**

**Presented for filing this 11.........day of 10.........2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 21275 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MESHAKI NDALIJE**

**DECEASED OF SOKOINE, DODOMA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AMON MESHACK NDALIJE PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATIONS**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 11 day of 11...................... 2024
Dated at Dodoma this 9......Day of 10...............2024

.....................................
**DISTRICT MAGISTRATE**

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kamala Harris aweka hadharani hali yake kiafya

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA urais wa chama cha Democrat, Kamala Harris ni amebainisha hali ya afya yake, ikibainika ni mwenye afya bora.

Licha ya majibu ya daktari wake kuonesha ana baadhi ya changamoto kiafya, amesema Kamala ana uthabiti wa mwili na kiakili.

Katika barua iliyoandikwa na daktari wa Harris, Joshua Simmons, anasema Makamu wa Rais wa nchi hiyo, ana historia ya mzio kwa msimu na urticaria (hali ya kawaida ya ngozi).

"Ana uthabiti wa mwili na kiakili, unaohitajikakuhudumu kama rais," daktari wake alisema katika barua.

Simmons anasema mizio yake imedhibitiwa vyema na dawa za dukani, ikiwa ni pamoja na dawa ya pua, matone ya macho na Allegra (kidonge cha mzio), lakini hazihitaji tena mara nyingi, baada ya miaka mitatu ya kinga ya allergen.

"Hakuwahi kupata dalili kali," anasema daktari huyo.

Kwa nini Harris alitoa rekodi zake za matibabu, wachambuzi wa kisiasa wanadai ni hatua ya kuongeza uaminifu kuelekea uchaguzi mkuu mwezi ujao.

Huku ikiwa imesalia chini ya mwezi mmoja kabla ya siku ya uchaguzi, Harris anafichua hali yake namatibabu, kuweka shinikizo kwa mpinzani wake, Trump.

Trump, mwenye umri wa miaka 78 na wa chama cha Republican, mara nyingi wamekuwa wakimshambulia Rais Joe Biden, kuwa mwenye umri wa miaka 81, kama mzee sana mara nyingi akimtaka afanye vipimo vya utambuzi wa afya yake.

Lakini kwa kuwa Harris ndiye mteule, Wanademokrasia wanatumai kubadilisha meza, wakitaka kutilia shaka umri wa Trump na kufaa kwa kazi hiyo.

*BBC*



Kamala Harris. **PICHA: MTANDAO**

# 'Hali ya kiutu Sudan ni ya kutisha'

**KHARTOUM, Sudan**

SHIRIKA la kutoa misaada la Madaktari wasio na Mipaka la MSF, limeelezea wasiwasi wake kuhusu hali inayowakabili watu wa Sudan.

Imetoia wito pande hasimu za mzozo huo ziruhusu misaada ya kiutu.

Wafanyakazi wa shirika hilo wameizungumzia hali ya Sudan wakati vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea nchini humo, vikisababisha ongezeko kubwa la utapiamlo na njaa.

Maeneo yenye mizozo hayafikiki kwa urahisi. Kwa Sudan, Shirika la Madaktari wasio na Mipaka la MSF ni miongoni mwa mashirika machache ya kimataifa ambayo bado yanaweza kufanya shughuli zake nchini humo.

Wakati lilipotoa taarifa yake jijini Nairobi, MSF lilisema kuwa, watu milioni 26 karibu sawa na nusu ya idadi jumla ya watu wa Sudan, wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula.

Katika taarifa hiyo mratibu wa shirika hilo, Claire San Filippo, alielezea hali ya utapiamlo nchini humo kuwa ni ya kuogofya.

Alitolea mfano wa mwanamke mmoja mwenye watoto watatu, ambaye ameshawapoteza wanafamilia wanane, kutokana na mzozo huo.

Aliyakimbia machafuko katika mji wa El-Fasher huko Darfur na alielezea kuwa mauaji na vita viko kila mahali.

Ilimchukua mwanamama huyo mwezi mmoja kutoka kwenye mji huo hadi kufika katika kambi ya wakimbizi mashariki mwa Chad.

*DW*

# Takribani 30 wauawa Gaza, mashambulizi ya Israel

**UKANDA WA GAZA, Gaza**

TAKRIBANI watu 29 wameuawa katika mashambulizi ya anga ya Israel katika eneo la kati na kaskazini mwa Ukanda wa Gaza.

Shirika la habari la Reuters limeripoti likiwanukuu madaktari.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), lilianza mashambulizi mengine huko Jabalia wiki moja iliyopita, likisema Hamas ilijaribu kurejesha miundombinu yake huko.

Takribani Wapalestina 150 wameuawa huko kwa muda wa wiki moja iliyopita, kulingana na maofisa wa afya huko Gaza.

Watu waliokimbia makazi yao katika eneo hilo, wanasema wanajeshi wa Israel wamezingira Jabalia na kuwaamuru kuondoka.

Kusini mwa Lebanon, Hezbollah inasema ilipambana na wanajeshi wa Israel wakijaribu kuhamia kijiji cha Ramiya, mapema Jumapili.

Wizara ya Afya ya Lebanon inasema watu 15 waliuawa katika mashambulizi matatu ya Israel huko Deir Bella, Al Maaysra na Barja.

Nchini Israel, IDF inasema Hezbollah ilirusha takribanI makombora 320 kutoka Lebanon hadi Israel siku ya Jumamosi. Waziri wa Ulinzi wa Israel: "Iran itajipata ikiwa kama Gaza na Lebanon"

*BBC*

# Washindi wa Tuzo ya Nobel waonya kuhusu nyuklia

**OSLO, Norway**

VIONGOZI wa Shirika la Nihon Hidankyo la manusurura wa mabomu ya atomiki, lililoshinda Tuzo ya Amani ya Nobel, wametoa onyo kuhusu hatari ya vita vya nyuklia kuongezeka.

Viongozi hao wametoa pia wito mpya wa kukomeshwa kwa silaha za nyuklia.

Mmoja wa walionusurika katika mashambulizi ya nyuklia yaliyofanywa na Marekani mwaka 1945 mjini Nagasaki, Shigemitsu Tanaka, amesema hali ya kimataifa inazidi kuwa mbaya na sasa vita vinaendeshwa, huku nchi zikitishia matumizi ya silaha za nyuklia.

Wakati wa kutoa tuzo hiyo, Kamati ya Nobel ya Norway, ilionyesha uharibifu uliotokana na milipuko ya atomiki ya Hiroshima na Nagasaki na kazi ya muda mrefu ya shirika hilo la Kijapani katika kutokomeza silaha za nyuklia duniani.

Tahadhari ya washindi hao wa tuzo ya amani ya Nobel imetolewa wiki kadhaa, tangu Rais wa Russia, Vladimir Putin, alipoashiria kuwa Moscow itaangalia uwezekano wa kufanya mashambulizi ya nyuklia, ikiwa Marekani na washirika wake watairuhusu Ukraine kuishambulia ndani kwa makombora ya masafa marefu yaliyotolewa na nchi za magharibi kwa Ukraine.

*DW*

# Waandamana kupinga ujenzi kinu cha nyuklia

**NAIROBI, Kenya**

BAADHI ya raia wameandamana kupinga pendekezo la kujenga kinu cha kwanza cha nyuklia katika Kaunti ya Kilifi, maarufu kwa utalii nchini Kenya.

Mwishoni mwa wiki, Shirika la Kiislamu la Kutetea Haki za Binadamu la MUHURI, liliyaongoza maandamano yaliyofanyika kuelekea ofisi ya Gavana wa Kaunti ya Kilifi, ambako waandamanaji walimkabidhi waraka wa kupinga mradi huo.

Mradi huo uliopendekezwa mwaka uliopita, umepangwa kutekelezwa mwaka 2027 na utaanza kufanya kazi mwaka 2034. Unatarajiwa kugharimu Shilingi za Kenya bilioni 500 sawa na dola bilioni 3.8 za Kimarekani.

Wengi wa wakazi wameonesha kulipinga waziwazi pendekezo hilo, wakihofia madhara yatakayosababishwa na kinu hicho cha nyuklia kwa raia.

Mara kadhaa maandamano hayo yamegeuka kuwa machafuko.

Kaunti ya Kilifi inafahamika kwa msitu wake ulio kwenye orodha ya urithi wa dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

*DW*

# Singida Black Stars yaitisha Namungo

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Singida Black Stars, Denis Kitambi, amesema timu yake iko tayari kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC utakaopigwa Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani, Singida.

Singida Black Stars ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 16 kibindoni wakati wageni Namungo yenye pointi sita iko katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo, timu hizo zimecheza mechi sita kila mmoja.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Simba yenye pointi 13 lakini imeshuka dimbani mechi tano na Fountain Gate iliyocheza michezo saba inafuatia ikiwa na pointi sawa na Wekundu wa Msimbazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kitambi, alisema malengo yake ni kuchukua pointi hizo na kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo na hatimaye kufikia malengo.

"Kwa sasa ninaendelea kuimarisha safu yangu hiyo kwa ajili ya kuhakikisha tunaendelea ushindani wetu katika mchezo wetu huo, alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema makosa ambayo waliyabaini katika michezo iliyopita wanaendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie katika mchezo huo unaofuata.

Aliongeza anaamini programu ya mazoezi aliyowaandalia wachezaji wake kuelekea ni nzuri kwa sababu inawaimarisha kuwa tayari kupambana kwa dakika zote za mchezo.

" Tunajua Namungo inaundwa na wachezaji wazuri, wenye uzoefu, lakini sisi hatuna wasiwasi na kikosi chetu kwa sababu vijana wanajitahidi kufuata maelekezo tunayowapa. Tutaingia tukiwa na tahadhari katika mchezo huo ambao utakuwa mgumu kwetu na kwa wapinzani, " alisema Kitambi.

Mabingwa watetezi Yanga yenye pointi 12, imecheza mechi nne mpaka sasa wako katika nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama kupisha Kalenda ya Kimataifa, itarejea tena kuanzia Oktoba 19, mwaka huu kwa Simba kuikaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# JKU YAGAWA POINTI Z'BAR, MASTRAIKA WAMLIZA KOCHA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC wameendelea kuandamwa na mzimu wa matokeo mabaya baada ya kupoteza mchezo wa pili mfululizo.

JKU ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wapinzani wao KVZ katika mchezo wa mzunguko wa sita wa Ligi Kuu Zanzibar, uliofanyika kwenye Uwanja wa New Amaan Complex.

Kwa matokeo hayo, JKU inashindwa kupata ushindi katika michezo yake mitatu, ikipata sare moja na ikiruhusu kufungwa mara mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKU, Salum Haji, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu licha ya timu hizo kuwa na ushindani kila zinapokutana.

Haji alisema timu wapinzani walipata faida ya kuondoka na pointi tatu muhimu katika dakika za nyongeza, kwa kufunga bao lililotokana na mabeki wake kushindwa kuelewana vyema.

"Hata hivyo licha ya upinzani uliokuwapo katika mchezo huo, timu yangu ilifanikiwa kumiliki mpira dakika zote za mchezo, lakini suala la kukosa umakini kwa washambuliaji wake lilipelekea kushindwa kutumia vyema nafasi za kupachika mabao tulizozitengeneza.

Licha ya presha ya mchezo wenyewe, lakini wachezaji walifanya kazi kubwa hasa ya umiliki wa mpira kwa muda mrefu, ni mchezo wa pili naona hili tatizo, ninaenda kulifanyia kazi katika uwanja wa mazoezi," alisema Haji.

Aliongeza ni hali ya kawaida kwa timu kupitia na 'upepo mbaya' wa matokeo lakini wanajipanga kupambana katika mechi zinazofuata na kurejesha heshima ya klabu yao.

"Ni upepo mbaya wa kupata matokeo tunaopitia, hii hali haitatuvunja moyo, nitawaandaa wachezaji wangu vyema kwa ajili ya mechi zinazofuata, nitawarejesha mchezoni ili kufanya vizuri, ninaamini tutarudi tukiwa tofauti," kocha huyo alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU yenye pointi 10 imebaki kwenye nafasi ya nne sawa na KVZ FC ambao wapo nafasi ya sita.



Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Polisi, Hamad Alli (katikati), akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Anmache katika mechi ya iliyochezwa kwenye Uwanja wa JMK Park jijini, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chess kamili kuibeba Tanzania

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya mchezo wa Chess yanatarajiwa kufanyika Oktoba 26 na 27, mwaka huu jijini, Dar es Salaam imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Chess Tanzania (TACA), Rashid Sharif, alisema mashindano hayo yatashirikisha wachezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Sharif alisema tayari usajili wa wachezaji umeshaanza na wanatarajia michuano ya mwaka huu itakuwa na ushindani kutokana na nyota wanaotarajia kuchuana.

"Mpaka sasa wachezaji kutoka Kenya, India na Ujerumani tayari wamethibitisha kushiriki, tunaamini tutakuwa na mashindano yenye upinzani mkubwa kwa sababu ya mwitikio wa washiriki, " alisema Sharif.

Aliongeza kwa kuwataka Watanzania wajifunze zaidi kuhusu mchezo huu kwa sababu pia unatoa fursa mbalimbali kwa vijana.

"Mashindano ya mwaka huu yatakuwa na mvuto kwa sababu kwa upande wa Tanzania tunatarajiwa kuwakilishwa na idadi kubwa ya wachezaji, lakini niwe mkwe maandalizi yao yamekuwa ya muda mrefu, hivyo tunatarajia watafanya vyema," Sharif aliongeza.

Alisema mchezo huu unachangamsha akili hasa kwa upande wa watoto na kuwaomba wazazi na walezi kuruhusu watoto wao wajifunze.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE KUUZWA JANUARI

KLABU ya Manchester United inajiandaa kumuuza mlinzi wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 31 katika diridha dogo la usajili la Januari. ***(Star)***

### HAALAND KUONDOKA CITY

MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland, mwenye umri wa miaka 24 ameamua kuhusu mustakabali wake mbali na Manchester City, lakini hatajiunga na Paris St-Germain. ***(El Nacional)***

### COSTA KUMRITHI EDERSON

MANCHESTER City imeonyesha nia ya kumsajili mlinda lango wa Ureno, Diogo Costa, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Porto kama mbadala wa muda mrefu wa Mbrazil Ederson (31). ***(Football Insider)***

### FERNANDEZ ATAJWA HISPANIA

REAL Madrid na Barcelona zinavutiwa na Mhispania mwenye umri wa miaka 21 anayeichezea Benfica ambaye ni beki wa zamani wa Manchester United, Alvaro Fernandez Carreras. ***(O Jogo)***

### GITTENS SOKONI ENGLAND

CHELSEA, Tottenham Hotspur na Liverpool ziemetuma maskauti kumtazama winga wa Borussia Dortmund na England wa umri chini ya umri wa miaka 21, Jamie Gittens, katika wiki za hivi karibuni. ***(Bild)***

### MAINOO, UNITED BADO

KIUNGO wa kati wa England, Kobbie Mainoo, mweye umri wa miaka 19, anasalia kwenye mjadala kuhusu mkataba mpya na Manchester United lakini hakuna makubaliano yaliyofikiwa.***(Fabrizio Roman***o)

### OMORODION AMTAJA MUNGU

MSHAMBULIAJI wa Porto na Hispania, Samu Omorodion, mwenye umri wa miaka 20 amesema Mungu ndiye aliyemfanya kushindwa kuhama kutoka Atletico Madrid na kujiunga na Chelsea msimu wa joto uliopita. ***(Metro)***

### BAYERN: HATUMTAKI BECKER

KLABU ya Bayern Munich haivutiwi na mlinda lango wa Liverpool na Brazil, Alisson Becker, mwenye umri wa miaka 32, licha ya mashaka kuhusu mustakabali wa Manuel Neuer katika klabu hiyo. ***(ESPN)***

### JAMES AITAMANI BARCA

MLINZI wa kulia wa Chelsea na England, Reece James, mwenye umri wa miaka 24, anatazama kupitia wawakilishi wake uwezekano wa kujiunga na Barcelona au Benfica. ***(Football Transfers)***

### KERKEZ, SEMENYO SOKONI

ARSENAL inapanga kuwasilisha dau la kumnunua beki wa kushoto wa Bournemouth na Hungary, Milos Kerkez, mwenye umri wa miaka 20, na winga Antoine Semenyo (24), ambaye ni mchezaji wa kimataifa kutoka Ghana. ***(CaughtOffside)***

### HOWE AIKATAA ENGLAND

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe mwenye umri wa miaka 46, hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo licha ya kuwa miongoni mwa watu walioorodheshwa kwa ajili ya kazi ya kuinoa England. ***(Telegraph)***

## DOND SOKA MAGAZ ULAYA




# MBAPPÉ ATETEWA KOSA LA 'KULA BATA'

## ●●●Nyota mwenzake asema ana uhuru wa kufanya chochote wakati wa...

**PARIS, Ufaransa**

WESLEY Fofana amejitokeza kumtetea nahodha wa Ufaransa, Kylian Mbappé, baada ya ripoti kuibuka mshambuliaji huyo wa Real Madrid alikuwa katika klabu ya usiku nchini Sweden wakati timu yake ikishinda dhidi ya Israel kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Mbappé tayari alikosolewa kwa kukacha mechi za Les Bleus dhidi ya Israel na Ubelgiji huku akiwa tayari kuichezea Real Madrid na jarida la Sweden la Aftonbladet liliripoti mchezaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain alikuwa kwenye klabu ya usiku jijini Stockholm huku wenzake wakihangaika kwenye ushindi wa mabao 4-1.

Fowadi huyo alipata jeraha la misuli Septemba, lakini akarejea uwanjani mapema kuliko ilivyopangwa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya Oktoba 2, mwaka huu wakati Madrid ilipopata kipigo cha kushtukiza kutoka kwa Lille, na kuanza mchezo wao uliofuata wa LaLiga dhidi ya Villarreal baada ya kuachwa nje ya kikosi cha Kocha, Didier Deschamps kwa kukosa maandalizi.

"Watu wanaweza kufanya wanavyotaka kwa muda wao wa mapumziko," alisema beki huyo wa Chelsea, Fofana akiwaambia waandishi wa habari.

„Sio jambo ambalo sisi kama kikosi cha Ufaransa tumezungumza kuhusu hilo, sikuwa nimesikia kuhusu hadithi hii.

"Anafanya kile anachotaka; yeye ni mtu mzuri na mtaalamu mzuri. Je, tunaifanya kupita kiasi? Sijui. Yeye ni mchezaji bora wa Ufaransa, hivyo ni kawaida inatangazwa sana.

"Nafikiri mara kwa mara vyombo vya habari huenda mbali kidogo. Unapaswa kumuuliza Kylian Mbappé kwa taarifa zaidi."

Kiungo wa kati wa Lazio, Matteo Guendouzi pia alizungumzia ripoti hizo alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari.

"Hatuna shaka kuhusu Kylian.... Hakuna swali kuhusu mapenzi yake kwa nchi yake," alisema.

"Anaipenda nchi yake, ataendelea kutusaidia, lazima tuache kuizungumzia sana.

"Ana siku za kupumzika; anaweza kufanya anachotaka."

Ufaransa inashika nafasi ya pili katika Kundi A2 la Ligi ya Mataifa ya Uefa na watacheza ugenini leo dhidi ya Ubelgiji.

# Ederson achambua nguvu ya Guardiola



**RIO DE JANEIRO, Brazil**

GOLIKIPA wa Brazil, Ederson amesema ana heshima kubwa kuwa sehemu ya mradi wa Pep Guardiola katika klabu ya Manchester City, lakini akakiri kocha huyo wa Hispania anaweza „kukukasirisha wakati mwingine.“

Éderson, akiwa katika majukumu ya kimataifa na Brazil, amefanya kazi chini ya Guardiola tangu 2017 na kushinda mataji 18, yakiwamo mataji sita ya Ligi Kuu England na moja ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alipokuwa akishiriki katika hafla ya siku ya Watoto nchini Brazili, Ederson aliulizwa na mtoto mmoja ikiwa Guardiola ni mzuri, anaudhi au ana hasira.

„Utaniingiza kwenye matatizo,“ alijibu Éderson mwenye umri wa miaka 31 akiambia ESPN Brasil.

„Yeye ni mtu mzuri, wakati mwingine anaudhi, kwa maana ya kudai sana kwa wachezaji na pia ana hasira.

„Kwa hivyo ana mchanganyiko wote. Lakini ni mtu mzuri nje ya uwanja na ni mtu anayehitaji sana jambo hilo. Na pia ni mtu ambaye hukasirika kama mtu mwingine yeyote, kama kocha mwingine yeyote.”

Tangu alipowasili City msimu wa joto wa 2016, Guardiola amechaguliwa kuwa kocha bora wa Ligi Kuu England mara tano.

Chini ya Guardiola, City ikawa mwaka 2023 klabu pekee ya England katika historia kushikilia mataji yote matano ( Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu na Kombe la FA England, Super Cup, Kombe la Klabu Bingwa Dunia katika mwaka wa kalenda.

Guardiola hapo awali alipata mafanikio katika kazi nzuri akiwa na Barcelona na Bayern Munich.

# Salah, Van Dijk kurejea mapema



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imethibitisha Mohamed Salah na Virgil van Dijk, watarejea kutoka kwenye majukumu ya kimataifa baada ya kuachiliwa na mataifa yao.

Salah hatashiriki katika mechi ya marudiano ya Misri dhidi ya Mauritania utakaochezwa kesho, licha ya kufunga bao katika michuano wao wa kufuzu kwa Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya timu hiyo Ijumaa iliyopita.

Juhudi za nyota huyo wa Liverpool zilihakikisha kikosi chake kinapata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani jijini Cairo.

Anatazamiwa kurejea Liverpool mapema kuliko ilivyotarajiwa, akiondoka kambini mwa taifa lake kabla ya mechi yao ya mwisho ya kimataifa.

Mholanzi Van Dijk pia ataondoka kwenye kambi ya taifa lake mapema baada ya kupata kadi mbili za njano katika sare ya 1-1 ya michuano ya Ligi ya mataifa ya Uefa dhidi ya Hungary.

Kupata kadi nyekundu kwa nahodha huyo wa Anfield, ilikuwa ni mara yake ya kwanza kwenye medani ya kimataifa na kumfanya asistahili kucheza mechi itakayofanyika leo dhidi ya Ujerumani.

Beki huyo alikiri hasira yake baada ya kuonyeshwa kadi mbili za njano na mwamuzi wa Uswisi, Lukas Fahndrich, akieleza baada ya mchezo huo: „Wanasema nahodha pekee ndiye anayeweza kuzungumza na mwamuzi. Mimi nilimfuata kinaonyeshwa kadi.”

Wawili hao watarejea Merseyside, lakini hawatarejea uwanjani hadi Liverpool watakapocheza na Chelsea kwenye Ligi Kuu England itakayofanyika Oktoba 20, mwaka huu.



# KOCHA BIELSA AJIBU TUHUMA ZA SUÁREZ

**MONTEVIDEO, Uruguay**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Marcelo Bielsa, amekiri mamlaka yake kuathiriwa na shutuma zilizotolewa na Luis Suárez mapema mwezi huu.

Fowadi huyo wa zamani wa Uruguay, alisema Bielsa alitengeneza mazingira magumu ya kazi wakati wa michuano ya Copa América ya 2024, kabla ya kuelezea ukosefu wa mawasiliano kati ya wakufunzi na wachezaji.

Suárez baadaye alifichua aliumizwa na kitendo cha kocha huyo na akawataka mashabiki wasiwageukie wachezaji kama „kitu kitaenda vibaya“.

Bielsa alizungumzia suala hilo hadharani kwa mara ya kwanza, baada ya Uruguay kufungwa bao 1-0 na Peru katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia kwa Ukanda wa CONMEBOL.

„Sijui kilichotokea na ninajua mamlaka yangu yameathiriwa kwa njia fulani,“ alisema Bielsa.

„Lakini nilijiandaa kwa mechi kwa umakini wa hali ya juu na majibu ya wachezaji yalikuwa sawa na nilipoanza kufanya kazi hapa. Haikubadilisha imani ambayo mechi iliandaliwa kwa njia yoyote.“

Kabla ya kushindwa, Rais wa Chama cha Soka cha Uruguay, Ignacio Alonso, aliahidi msaada wake kamili kwa Bielsa na akasisitiza kocha huyo anasalia kuwa sehemu muhimu ya mradi wa kuelekea Kombe la Dunia la 2026, kama alivyofanya alipowasili Mei, mwaka jana.

„Sawa, alichosema Luis ni kweli, ameniambia na Jorge Giordano pia,“ alisema Alonso akikiambia kipindi cha De fútbol se habla así kwenye televiesheni ya DirecTV.

„Kuna mabadiliko kutoka enzi moja hadi nyingine, na kizazi ambacho kinaingia na urithi wa ajabu na tunaweka dau kwa Marcelo Bielsa, kama kiongozi wa soka, anaweza kuwa mtu bora kwa timu yetu,“ aliongeza Alonso.

Licha ya kupoteza, Uruguay inashika nafasi ya tatu ya msimamo wa kundi lao na pointi 15 katika michezo tisa waliyocheza.

Timu sita bora zitafuzu moja kwa moja Kombe la Dunia, huku nafasi ya saba ikilazimika kushiriki mechi ya mchujo.

HABARI MICHEZO

# FOUNTAIN GATE, DODOMA JIJI MAWINDONI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

FOUNTAIN Gate imeitumia salamu KMC kuwa haitakubali kupoteza mechi kwa mara ya pili mfululizo, baada ya kufungwa mabao 3-2 dhidi ya Prisons katika mchezo uliopita.

Mechi hiyo itachezwa Oktoba 20, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mkoani Manyara, ambao Fountain Gate inautumia kama uwanja wake wa nyumbani.

Ofisa Habari wa Fountain Gate, Issa Mbuzi, aliliambia gazeti hili wamepata bahati mbaya ya kwenda katika mchezo huo ugenini, huku wenyeji wao wakitoka kujeruhiwa.

“Ni bahati mbaya sana kwa KMC, wanakuja kucheza na sisi wakati wametoka kufungwa na Prisons, mchezo huo tunacheza nyumbani na hatutakubali kupoteza kama ilivyo kawaida yetu, hatujawahi kupoteza mchezo wowote kwenye uwanja huo,“ alisema Mbuzi.

Fountain Gate, imecheza mechi saba za Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, ikishinda mechi nne, sare moja na kupoteza mbili, ikikamata nafasi ya tatu ikiwa na pointi 13 kibindoni wakati KMC wanashika nafasi ya nane, ikicheza michezo saba, ikishinda miwili, sare miwili na kupoteza mitatu, ikiwa na pointi nane mkononi.

Wakati huo huo, Dodoma Jiji inaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuifuata Coastal Union katika mchezo utakaofanyika Ijumaa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Nizar Khalfan, alisema jana kikosi hicho kimeanza mazoezi kwa kazi moja tu kuhakikisha wanashinda mchezo huo, ili kukaribia malengo.

“Michezo saba tuliyocheza bado haijatuharibia malengo, tuko palepale kuhakikisha msimu ujao tunacheza mechi za kimataifa kwa kushika nafasi nne za juu,“ Nizar alisema.

Aliongeza wanashukuru kikosi chao hakina wachezaji ambao wana majeraha makubwa, baadhi ambayo ni majeruhi, wanaendelea vizuri na siku chache wanatarajia kuungana na wenzao.

“Tuna Ibrahim Ajibu ambaye alipata majeraha katika mchezo dhidi ya Simba, halafu nahodha wetu, Hassan Mwaterema naye ni mgonjwa, lakini hawa wote hali zao zinaendelea vizuri tunaamini mpaka Ijumaa watakuwa sawa, hata kama hawakucheza mechi dhidi ya Coastal Union, basi watacheza mchezo unaofuata dhidi ya JKT Tanzania,“ aliongeza kocha huyo.



Wachezaji wa Mtibwa Sugar wakishangilia bao katika mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Songea United ya Ruvuma iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro Ijumaa. Mtibwa Sugar ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba Queens, Yanga kazini

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi, Simba Queens wanatarajia kuikaribisha Fountain Gate Primcess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake itakayochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex Dar es Salaam.

Simba Queens ilianza vyema msimu mpya kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mlanzidi Queens ya Pwani ambayo imerejea tena katika ligi hiyo.

Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan ‚Mgosi‘ ameliambia gazeti hili hakuna mechi rahisi katika ligi hiyo na kikosi chake kimejipanga imara kusaka ushindi.

Mgosi alisema wameendelea kufanyia kazi makosa na anaamini leo watawapa burudani nzuri mashabiki wao.

Naye Ofisa Habari wa Fountain Gate Princess, Issa Mbuzi, alitamba wataingia katika mechi hiyo wakiamini wanaenda kuchukua pointi tatu na si matokeo tofauti na ushindi.

“Tumejipanga, tunawaambia Simba Queens wajipange, watakutana na kikosi bora na kilichojiandaa kuwania ubingwa msimu huu,“ alitamba Mbuzi.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni Alliance Girls itawaalika Yanga Princess wakati Mlandizi Queens itaivaa Gets Program, Mashujaa itakutana na Ceasiaa huku Bunda ikivaana na JKT Queens.

## Yanga yaanika siri inapowazidi Simba

INATOKA UK. 24

obeba hisia, lakini una pointi tatu tu, utofauti ni uhasimu tu uliopo, hii ni ligi yenye michezo 30, hata kama tukishindwa kupata matokeo mazuri, tunaweza kucheza mechi nyingine tukashinda, tukawa mabingwa,“ meneja huyo aliongeza.

Alisema pia suala la kuwapa ahadi endapo watashinda mechi hiyo kwao hufanyika katika kila mchezo lakini ni huwa ni siri baina ya klabu na wachezaji.

“Sisi kila mchezo tunahamasishana wenyewe kwa wenyewe na ahadi huwa ni siri, si tunafanya katika mchezo huu wa dabi, bali ni kwa ligi nzima, kila mechi kwetu ni muhimu,“ alifafanua Harrison.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana katika mechi ya hatua ya nusu Fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Agosti 8, mwaka huu, Yanga ikishinda bao 1-0 shukrani kwa Mkongomani, Maxi Nzengeli.

Yanga ambayo ina pointi 12, imecheza mechi nne mpaka sasa iko katika nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Watani zao Simba wamejikusanyia pointi 13 baada ya kucheza michezo mitano wakati vinara wa ligi hiyo ni Singida Black Stars yenye pointi 16 lakini imeshuka dimbani mara saba.

Ligi hiyo ilisimama kupisha Kalenda ya Kimataifa, ambapo kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wenyeji Taifa Stars wataikaribisha Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025).

## Che Malone ataka umakini

INATOKA UK. 24

tunaenda kucheza naye, ili kupata matokeo ni lazima wanachama mashabiki, viongozi na wachezaji tukapambane, tujitoe na tushirikiane kweli kweli.

Hii si mechi ya viongozi na wachezaji peke yao, au benchi la ufundi, ni mechi ya Wanasimba wote, tunapaswa kuingia msituni, kuhakikisha tunasaidia, hii ni mechi ya kitamaduni, tunacheza na mkubwa mwenzetu, tukicheza mechi nyingine, hizo ni za wachezaji, benchi la ufundi na viongozi, lakini sio hii,“ alisema Ahmed.

Simba itaingia katika mchezo huo ikiwa na pointi 13 baada ya kushinda meci nne na kutoka sare moja wakati Yanga imeshinda michezo yake yote minne iliyocheza msimu huu.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 14, 2024

Nipashe


**Mbappé atetewa kosa la 'kula bata'**

UKURASA 22



# YANGA YAANIKA SIRI INAPOWAZIDI SIMBA

## ●●●Yatamba ubora, uzoefu wa nyota walioko katika kikosi chake pamoja...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga imetamba sababu kubwa inayowapa ushindi katika mechi za dabi kwa siku za karibuni ni kutokana na kikosi chake kuundwa na wachezaji wengi wazoefu na wanaotambua umuhimu wa michezo hiyo.

Yanga itashuka ugenini katika mechi ya watani wa jadi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Meneja wa Yanga, Walter Harrson, aliliambia gazeti hili uwezo na juhudi za wachezaji wao ambao wanajipanga kucheza katika viwango vya juu pamoja na kuonyesha ,vitu' walivyonavyo mbele ya mashabiki wao husaidia kupata matokeo chanya.

Harrison alisema wao kama viongozi linapokuja suala la mechi ya dabi huwa hawazungumzi sana kwa sababu mechi yenyewe inajieleza na kila mchezaji anajiandaa vyema kisaikolojia kutimiza majukumu yake.

Meneja huyo alisema kila mchezaji anajua anachotakiwa kukifanya katika mchezo huo na wanafahamu kiwango bora huwasaidia kujiongezea thamani na umaarufu lakini wakijua pia wanajiweka sokoni.

"Tumekuwa tukipata ushindi kwa siku za hivi karubuni tukicheza dhidi ya Simba, kikubwa kwetu viongozi mechi hii hatuhitaji kuhamasisha sana kama michezo mingine ambayo wachezaji wanakuwa wamejisahau au wanazichukulia kawaida.

Kwa kiasi kikubwa wachezaji wetu wengi wameshacheza mechi hizi, hawahitaji sana kuelezwa, hakuna asiyefahamu ukubwa wa dabi. Wenyewe wanajiandaa na kila mmoja anataka kupata nafasi ili aonyeshe alichonacho akijua ataangaliwa na watu wengi uwanjani na kupitia televisheni, kwa hiyo haiitaji sana kuizungumza, yenyewe inajizungumza," alisema Harrison.

Kuhusu maandalizi, meneja huyo alisema wanaendelea na mazoezi na kufanyia maboresho makosa ambayo waliyabaini katika michezo iliyotangulia ili kuhakikisha wanaendeleza ubabe dhidi ya Simba.

"Tuko katika maandalizi makali, tunaweka kila juhudi inayotakiwa kuhakikisha tunashinda. Huu ni mchezo mkubwa una-

INAENDELEA UK. 23



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa ( Taifa Stars), Bakari Mwamnyeto (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa kuikabili Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Che Malone ataka umakini

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa kati ya Simba, Che Malone Fondoh, amewaonya wachezaji wenzake kuhakikisha wanazidisha umakini na kutofanya makosa kuelekea mechi ya watani wa jadi itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Che Malone amesema hayo kufuatia sare ya mabao 2-2 waliyopata dhidi ya Coastal Union.

Beki huyo alisema endapo watarudia makosa, timu yao inaweza kupata matokeo mabaya ambayo yatawaathiri kuelekea katika mbio za ubingwa msimu huu.

Nyota huyo raia wa Cameroon, amesema wachezaji wengi waliharibiwa ,karia' zao katika soka kutokana na mechi za dabi, hivyo anawaomba nyota wenzake wa Simba kutuliza akili, wacheze kwa bidii, wapambane na kuhakikisha wanailetea timu yao ushindi.

"Mechi ya Yanga ni fainali kwetu, hasa sisi wachezaji ni michezo ambayo inaweza kukufanya mchezaji ukawa staa zaidi kama mkipambana na timu kupata usindi au kuathiriwa kisailojia kama ikipoteza, tunatakiwa tutulize akili zetu na kucheza kwa bidii, kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema mchezaji huyo ambaye ana msimu wa pili katika kikosi cha Wekundu wa Msimbazi baada ya kusajiliwa akitokea Coton Sport ya Cameroon.

Aliongeza haamini kama wanaweza kurudia makosa kwa sababu ya ukubwa uliopo wa mechi ya dabi tofauti na walivyocheza dhidi ya Coastal Union.

"Katika mechi dhidi ya Coastal Union tumeruhusu mabao rahisi, tunatakiwa tubadilike, tusifanye tena makosa kama yale na nadhani haitatokea kwa sababu tunakwenda kucheza na Yanga, Coastal Union si wabaya, tumetoka sare na imetukumbusha tusidharau mechi, zote tuzichukulie kwa uzani sawa," aliongeza beki huyo.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamejipanga vyema ili kushinda dabi hiyo na kurejesha amani na heshima ya klabu yao.

"Lazima tuelezane ukweli, hii ni mechi ngumu kulingana na mpinzani ambaye

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA

9 770856 541002